epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com
Nipashe
Alhamisi Desemba 5, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581881
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII
Nipashe digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710
LIKE & FOLLOW US

# Warioba atema cheche



• **Asema** Rais asihusishwe, alishatoa msimamo... *EndeleaUkurasa 3*



Watu wanaotuhumiwa kumteka mfanyabiashara, Deogratius Tarimo, katika eneo ya Kiluvya hivi karibuni, wakishuka kwenye gari la polisi katika Kituo cha Kati, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kukamatwa na jeshi hilo. **Picha ndogo:** Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, SACP Jumanne Muliro, akionyesha kwa waandishi wa habari, gari aina ya Toyota Raum, lililotumiwa na watuhumiwa hao. **PICHA ZOTE: IMANI NATHANIEL**

## Matatani kwa madai jaribio la kuteka mfanyabiashara Tarimo

UK. 2

UKURASA WA 3

**Mapya** yaibuka kutekwa kwa Nondo



UKURASA WA 4



**Rais** Samia afuta sherehe za miaka 63 ya Uhuru wa Bara

UKURASA WA 4

**Mbaroni** tuhuma mauaji mwenyekiti UVCCM, mkulima

**Gumzo kila kona kuhusu kukwama kwa treni ya SGR**

UKURASA 2

**MICHEZO** **FEI TOTO HAKAMATIKI ASISTI, MABAO YA PENALTI** UK.23

**MAONI,** UK.6

# Matatani madai kumteka mfanyabiashara Tarimo

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limesema linashikilia kundi la watu wanane wanaotuhumiwa kula njama na kufanya tukio la kumteka Deogratius Tarimo.

Tukio hilo lilitokea Novemba 11, mwaka huu, eneo la Kiluvya, Ubungo, Dar es Salaam, ambapo kupitia video fupi iliyosambaa mtandaoni, ilionesha namna watuhumiwa wakimlazimisha Tarimo kuingia katika gari ndogo, huku wananchi wakishuhudia.

Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, akizungumzia jana kuhusu operesheni maalum ya kuzuia vitendo vya uhalifu waliyofanya, alisema wanawashikilia watu wanane katika tukio hilo.

"Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limekamata kundi la wahalifu wanane wanaotuhumiwa kula njama kwa pamoja na baadaye kufanya tukio la kumteka Deogratius Tarimo.

"Watuhumiwa hao wamekamatwa kwa nyakati tofauti Dar es Salaam, Songea, Ruvuma na eneo la Mbingu Mlimba, Morogoro. Limepatikana gari aina ya Toyota Raum ambayo lilitumika wakati wa tukio hilo," alisema.

Kamanda Muliro alisema wakati wa tukio hilo, gari hilo liliwekwa namba isiyo halisi T 237 EGE na baada ya ufuatiliaji wamebaini namba yake halisi ni T 237 ECF.

Aliwataja watuhumiwa hao ni Bato Tweve (32), bondia (32) mkazi wa Kimara Bunyokwa, Yusuph Abdalla (32) mkazi wa Mbingu, Mlimba, Morogoro, Fredrick Juma (31) mkazi wa Kibamba, Dar es Salaam na Nelson Elimusa (24) maarufu msela dereva teksi, mkazi wa Mbezi Luguluni.

Wengine ni Benk Mwakalebela (40) maarufu tall mkazi wa Mbezi Makabe, Lusungo, Mbeya, Thomas Mwakagile (45) maarufu baba mage mkazi wa Bunyokwa, Mbeya, Anitha Temba (27) mkazi wa Mbezi Mwisho na Isack Mwaifani maarufu boxer mkazi wa Kimara Temboni Salanga.

Kamanda Muliro alisema Jeshi la Polisi linaendelea na kazi ya kuzuia vitendo vya kihalifu, pia kuwakamata na kutokuwa na huruma kwa watuhumiwa wote wanaojihusisha na matukio ya uhalifu.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***


TANGAZO LA MKUTANO MKUU WA MWISHO WA WANAHISA WA KAMPUNI YA

TSCHUDI TANZANIA LIMITED

**Cheti cha Usajili No. 155877022**

Sheria ya Makampuni, 2002 (Kifungu 334 (1))

Umma na wahusika wanafahamishwa kutakua na mkutano mkuu wa mwisho wa wanahisa wa kampuni TSCHUDI TANZANIA LIMITED, yenye usajili namba **155877022** kitakachofanyika tarehe 30 December 2024 ofisini kwa mfilisi saa 4:30 asubuhi ambapo mfilisi atatoa hesabu ya kufungwa kwa hiari kwa kampuni.

| | |
|---|---|
| Mfilisi | NEEMA RICHARD |
| Amwani ya Mfilisi | 368 MSASANI ROAD<br>MIKUMI HOUSE<br>OYSTERBAY<br>P.O BOX 9673<br>DAR ES SALAAM<br>TANZANIA |
| Tarehe ya kuchaguliwa | 2 OCTOBER 2024 |
| Amechaguliwa na | WAMILIKI WA KAMPUNI |

Sahihi ........................................................ **Tarehe: 29/11/2024**

**Jina: NEEMA RICHARD**

182826



Lindi Jumbo Limited

JOB VACANCY

PLANT ENGINEER

Location: Matambarale, Ruangwa District, Tanzania.
Closing Date : 20 December 2024, 4:00PM (GMT+2)
To apply and view more details visit: https://jobportunities.net/jobs_search.aspx



For assistance on the portal, please contact the Tara Nawa team at +264 (0)64 402403 or WhatsApp +264812294611. Alternatively send an email via the recruitment portal's Contact Us page.

182841


# Gumzo kila kona kuhusu kukwama treni ya SGR

**Na Halfani Chusi**

GUMZO liliibuka jana kutoka kwa wadau mbalimbali baada ya treni ya mwendokasi (SGR) kukwama kwa muda, huku sababu ikitajwa kuwa ni hitilafu ya umeme katika Mfumo wa Gridi ya Taifa.

Kutokana na hali hiyo, wadau wameshauri kuwe na njia mbadala ya umeme ili ukikatika usiathiri huduma hiyo.

Jana, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lilitangaza kuwapo kwa hitilafu iliyojitokeza katika Mfumo wa Gridi ya Taifa, huku Shirika la Reli Tanzania (TRC) likieleza kuwa imesababisha kusimama ghafla kwa treni za mwendokasi zilizokuwa safarini kati ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma.

Baadhi ya wadau waliozungumza na Nipashe, walishauri ili changamoto hiyo isijitokeze katika mradi huo wa kisasa SGR ni vyema kuwe njia mbadala ya umeme.

Mkuu wa Shule ya Mafunzo ya Anga wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) Mabibo, Dar es Salaam, Denis Mwageni, katika maoni yake, alishauri TRC kushirikiana na TANESCO kuweka njia mbadala ya umeme ili unapokatika safari za treni zisikwame.

Mwageni alishauri TANESCO itengeneze mfumo ambao utawasaidia kutoka katika chanzo kikuu ambacho kitakuwa na uhakika na kutoathiri SGR.

Alishauri pia ili kukabiliana na changamoto ya namna hiyo, wampe mwekezaji anayeweza kuwapatia umeme mkamilifu kwa ajili ya kusaidia kuendesha SGR.

"Lakini kama umeme utakuwa hautoshi kiasi cha kuendesha SGR bila kukatika, wanaweza kununua kutoka nchi jirani kama Ethiopia ambao wana umeme wa kutosha na uelekezwe moja kwa moja kwenye eneo hilo, ninaamini hiyo itakuwa suluhu ya kusimama kwa SGR kutokana na kukatika kwa umeme," alishauri Mwageni.

Baada ya hitilafu hiyo, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano TRC, Fredy Mwanjala, akizungumza na Nipashe, alisema mbali na treni hiyo kupoteza muda wa abiria, hakuna aliyepata athari yoyote.

Kwa mujibu wa taarifa iliyosainiwa na Mwanjala, "abiria walioathirika kutokana na kukatika kwa umeme huo ni wale walioanza safari yao saa 2:00 asubuhi kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma.

"Abiria wa treni ya saa 3:30 kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma na abiria waliotoka na treni ya 3:50 kutoka Morogoro kwenda Dar es Salaam," alisema.

Mwanmjala alisema jitihada zilizofanyika zimesaidia umeme kurejea saa 5.30 asubuhi na safari ikarejea kama kawaida.

Kutokana na changamoto hiyo, shirika hilo limeomba radhi abiria kwa usumbufu uliojitokeza.

Aidha, taarifa iliyotolewa na TANESCO, ilisema changamoto hiyo imesababisha mikoa inayopata umeme kutoka Gridi ya Taifa kukosa huduma hiyo, hivyo wataalamu wanaendelea na uchunguzi kubaini chanzo cha hitilafu hiyo.

"Umeme kwa sasa umeanza kurejea kwa awamu katika mikoa iliyokuwa inakosa umeme na jitihada zinaendelea kuhakikisha mikoa yote inapata huduma hii mapema iwezekanavyo," ilisema taarifa hiyo iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano na Huduma kwa Wateja TANESCO.

Shirika hilo limeomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza na kuahidi kuendelea kutoa taarifa za hali ya urejeshaji wa huduma kadri zinavyoimarika.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Jaji Warioba atema cheche

**Elizabeth Zaya na Restuta James**

WAZIRI Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais mstaafu, Jaji Joseph Warioba, ametema nyongo akionya kuhusu matumizi mabaya ya vyombo vya dola, dosari kwenye uchaguzi, utekaji na mauaji.

Sambamba na hilo, amegusia uchaguzi mkuu ujao na kuhadharisha kuwa endapo serikali haitachukua hatua madhubuti, kuna hatari ya kutokea mgawanyiko miongoni mwa Watanzania, hivyo kuharibu amani ya nchi.

Akizungumza jana Dar es Salaam katika mkutano wake na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Jaji Warioba alisema baadhi ya mambo yanayoendelea yanahatarisha amani ya nchi.

Kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika mwishoni mwa mwezi uliopita, alisema wananchi waliamini ungekuwa tofauti na ilivyotokea mwaka 2019, lakini hali imekuwa ile ile.

Jaji Warioba alisema Rais katika hilo asihusishwa kwa sababu alishatoa msimamo kwamba anataka ucuaguzi uwe huru na haki.

"Na yametokea yale yale na chanzo chake zaidi ni wasimamizi wa uchaguzi. Kama tutaendelea na utaratibu huu, tunajenga mazingira ya vurugu ambayo itahatarisha amani yetu," alisema.

Alisema tatizo kubwa ni kuenguliwa kwa wagombea wengi wa vyama vya upinzani, kwa madai ya kujaza fomu vibaya na kukiuka utaratibu na kutoa taswira kwamba wagombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) walikuwa vizuri.

"Haiwezekani, wananchi waamini kwamba walioenguliwa walikosea, lakini wanaoenguliwa ni wa upande mmoja kwamba kuna vyama ambavyo wagombea wake wanajua na wanafuata masharti na kuna vyama ambavyo wagombea wake hawajui.

"Hapa nazungumzia Watanzania wa kawaida kabisa. Haiwezekani na wala tusije tukadanganyika kwamba kuna maelezo ya sababu ya watu kuenguliwa hawakufuata masharti. Tutakuwa tunajidanganya tukiamini hivyo," alisema

Alisema uchaguzi wa mwaka 1995, ulileta mgawanyiko uliosababisha matatizo visiwani Zanzibar, chuki na uadui na kwamba alishirikiana na wenzake kutoa ushauri kwa viongozi kwamba wasiache hali hiyo iendelee.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, Jaji Warioba alisema ni vyema mamlaka zinazohusika kusimamia uchaguzi zikachukua hatua kuhakikisha unafanyika vizuri.

"Lakini ninavyoona ukiona mjadala wote uliofanywa tangu mwaka 2019 mpaka sasa, na imani iliyokuwapo kwa uchaguzi wa mwaka huu hautofautiani na ule wa mwaka 2019. Matokeo yake, uchaguzi wa mwaka kesho, utakuwa ni vilevile, kama tusipochukua hatua utakuwa kama huu uliopita.

"Kwa nini tume itakayosimamia uchaguzi wa mwaka kesho, ni ile ile iliyosimamia uchaguzi wa mwaka 2020? Maana sioni dalili pamoja na sheria kupitishwa kwamba uwe na tume tofauti. Sioni dalili kama tume hiyo itaanzishwa kabla ya uchaguzi.

"Kwa hiyo ni tume hii itakayoendesha uchaguzi wa mwaka kesho, watakaosimamia ni wale wale ambao wapo chini ya Tamisemi, uongozi wa kisiasa ni uleule ndani ya Tamisemi, sioni kama hawakusikiliza haya yaliyosema katika kipindi chote hiki na wakarudia ya zamani, hata mwaka kesho watafanya vilevile," alisema.

Jaji Warioba alisema ni vyema hatua zaidi zikachukuliwa kuepusha na kudhibiti kasoro zinazojitokeza katika chaguzi hizo.

"Bila kufanya hivyo tutakuta watu wanaenguliwa wengi, tutakuta kura za bandia, na mengine yanaofanana, tukifanya hivyo ni lazima kama taifa tuangalie cha kufanya kuhakikisha hayo yasiendelee.

"Moja ni kumuomba Rais, kwa kweli achukue hatua, haya matatizo tuliyonayo kwa kiwango kikubwa, yanamwitaji Rais kuchukua hatua, kama kuna umuhimu wa kuzungumza tuzungumze, mimi naogopa kabisa tukiendelea hivi, amani tuliyonayo itavunjika na hakuna kitu ambacho ni cha msingi katika nchi hii kama amani tuliyonayo. "Na amani hiyo inatokana na mshikamano wetu, tukianza kuvuruga umoja wetu, amani itaanza kutoweka. Kwa hiyo nikushauri kwamba tujue tunalo tatizo kubwa, pili tatizo hilo linataka serikali ichukue hatua ambayo inaweza kutatua tatizo,"alisema.

Akijibu maswali maswali alipoulizwa kuhusu ripoti iliyotolewa na serikali baada ya uchaguzi, Jaji Warioba alisema: "Nimeona serikali Inasema imefanikiwa asilimia 100 kwenye uchaguzi huu, unasemaje umefanikiwa asilimia 100 wakati tunapoteza watu, hili lilinistua...na kwa kweli ninayosema ma ninaogopa yanaweza kutokea tena.

"Kwa hiyo tukisema turudi kwenye mwenge, tuseme uwe na matumaini lakini kuna watu wanaanza kukata tamaa, tuwe na upendo lakini wanaanza kuharibu, tuwe na hekina lakini kuna watu wanaleta chuki.

Kuhusu Jeshi la Polisi, Jaji Warioba alisema: "Polisi nacho ni chombo muhimu sana na ndicho kinalinda wananchi na mali zao na kinatakiwa kifanye kazi na wananchi wote. Katika miaka michache iliyopita tumeliingiza Jeshi la Polisi katika siasa.

"Linatoa matamko ya kisiasa, na hii italeta mgawanyiko, wananchi watagawanyika, tuliache Jeshi la Polisi lifanye kazi zake za kawaida. Na bahati nzuri Rais (Samia Suluhu Hassan), aliona malalamiko ya wananchi, akaona wamepoteza imani, akaunda tume ambayo ilipendekeza Jeshi hilo liachwe lifanye kazi yake. Lakini sasa hivi tumeliingiza kwenye siasa,' alisema.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

## Mapya yaibuka kutekwa kwa Nondo

**Na Restuta James**

MAPYA yameibuka siku nne baada ya kutekwa kwa Mwenyekiti wa Taifa wa Ngome ya Vijana wa ACT-Wazalendo, Abdul Nondo, chama hicho kikidai kuwa kiongozi huyo amekutwa na kiwango kikubwa cha sumu mwilini.

Aidha, madaktari wanaendelea kufanya uchunguzi wa kitabibu ili kubaini aina ya sumu hiyo.

Katibu wa Habari na Uenezi wa ngome ya vijana wa chama hicho, Philibert Macheyeki, alisema jana katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, kuwa mbali na sumu, madaktari wamemfanyia upasuaji mdogo kwenye unyayo. "Madaktari wamedai mwili wa Abdul Nondo unaonesha kuwa na kiwango kikubwa cha sumu, ambayo mpaka sasa hawajajua kama zimetokana na athari za kupigwa na kuteswa au kama alipewa kitu chenye sumu na watekaji wake," alisema katika taarifa hiyo.

"Uongozi wa ACT-Wazalendo Taifa, umewaomba madaktari kumfanyia uchunguzi zaidi kwa ajili ya kubaini aina ya sumu iliyo mwilini mwake na kama zimetokana na kupewa sumu kwa sasa hali yake bado sio nzuri, mikono yake imevimba na ana maumivu makali mwilini japo madaktari wanaendelea kupambana kuhakikisha afya yake inaimarika na kurudi kwenye hali yake ya kawaida."

Macheyeki alisema Nondo alifanyiwa upasuaji wa unyayo juzi Desemba 3, 2024 baada ya madaktari wa Hospitali ya Aga Khan, alikolazwa kubaini uwepo wa mivunjiko midogomidogo.

Alisema tatizo hilo limesababishwa na kipigo alichofanyiwa na watekaji ambao walimtupa katika ufukwe wa Coco Beach, Dar es Salaam.

Nondo anadaiwa kutekwa Desemba Mosi, mwaka huu kwenye Stendi ya Mabasi ya Magufuli, wilayani Ubungo, Mkoa wa Dar es Salaam, akitokea Kigoma alikoendesha kampeni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Alidai alichukuliwa kwa nguvu na watu sita, ambao walimfunga mikono na miguu na kumfunika uso kwa kitambaa cheusi na baadaye kumpiga sehemu mbalimbali za mwili wake.


Nipashe
WhatsApp Chaneli
Skani hapa kutembelea chaneli yetu



The Guardian Limited

VACANCY

Sales Freelancer

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales Freelancer to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, ( Moshi, Arusha, Tanga, Morogoro, Iringa, Mwanza and Zanzibar)**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

182777

**Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15st December, 2024.**

# Rais Samia afuta sherehe za Uhuru

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amefuta maadhimisho ya sherehe za miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara kwa mwaka 2024 na kuelekeza yafanyike katika ngazi ya mikoa.

Licha ya kufuta maadhimisho hayo, Rais Samia ameelekeza fedha zilizotengwa katika kila taasisi kwa ajili hiyo, zielekezwe katika kutoa huduma za kijamii.

Pia ameelekeza kila mkoa uhakikishe wilaya zake zinafanya shughuli za kijamii ikiwamo upandaji miti, usafi wa mazingira katika maeneo ya kijamii kama vile masoko, hospitali, kambi za wazee na wenye mahitaji maalum.

Kadhalika, ameagiza kufanya mashindano ya michezo mbalimbali pamoja na makongamano na midahalo ya kujadili maendeleo endelevu ambayo nchi imefikia katika kipindi cha miaka 63 ya Uhuru.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema hayo jana jijini Dodoma katika kikao kazi cha mawaziri kilichofanyika katika ukumbi wa Hazina.

"Sherehe za mwaka huu hazitakuwa na gwaride na shughuli zingine za kitaifa," alisema Waziri Mkuu Majaliwa.

Badala yake, alisema serikali inatoa wito kwa wananchi kushiriki katika shughuli hizo ili kujivunia sifa za kipekee ambazo zimetokana na Uhuru.

"Ninatoa rai kwa wakuu wote wa mikoa kuzingatia na kufuata ipasavyo maelekezo mahsusi yaliyotolewa na serikali ili kuhakikisha maadhimisho haya yanafanyika kwa ufanisi kwa lengo la kuuenzi Uhuru wetu," alisema.

Majaliwa alisema shughuli za maadhimisho zilishaanza tangu mwanzoni mwa mwezi huu na zitafanyika hadi siku ya kilele ambacho ni Desemba 9, mwaka huu. "Katika maadhimisho haya, taasisi zote za serikali na vyombo vyote vya ulinzi na usalama zinaelekezwa kuhakikisha majengo yote ya serikali Tanzania Bara yanapambwa kwa vitambaa vya rangi ya bendera ya Taifa.

"Picha rasmi ya Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye ni Muasisi wa Uhuru wetu pamoja na picha ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ziwekwe," alisema.

Maadhimisho hayo yanabebwa na kauli mbiu isemayo "Miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara: "Uongozi madhubuti na ushirikishwaji wa wananchi ni msingi wa maendeleo yetu"

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@ guardian.co.tz***



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (kulia), akizungumza wakati akifungua mkutano wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika Tawi la Tanzania (Misa-Tan), jijini Dodoma jana. Wa pili kulia ni Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Salome Kitomari. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbaroni tuhuma mauaji wenyeviti UVCCM, mkulima

**Na Grace Mwakalinga**

JESHI la Polisi, linawashikilia watu watano kwa tuhuma za mauaji akiwamo Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) Tawi la Machinjioni, Chunya mkoani Mbeya, Michael Kalinga (36) na Isack Malya (71), Mkulima na mkazi wa kijiji cha Kibosho Umbwe Onana, Moshi, Kilimanjaro.

Mkoani Mbeya, jeshi hilo linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za mauaji ya aliyekuwa Mwenyekiti wa UVCCM, Michael Kalinga (36), Mkazi wa Makongolosi, Chunya kwa kumpiga na kitu butu kichwani.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi (ACP) Wilbert Siwa, jana alithibitisha kukamatwa kwa watuhumiwa hao.

Alisema tukio hilo lilitokea Desemba 2, mwaka huu, majira ya saa 5:30 usiku eneo la Mikoroshini wilayani Chunya.

Kamanda Siwa alisema Kalinga alikutwa amefariki dunia na mwili wake kutelekezwa porini umbali wa mita 250 kutoka barabara ya Makongolosi Kwenda Lupa Tingatinga.

Alisema mwili wa marehemu ulikutwa na majeraha kichwani sehemu ya utosini kutokana na kupigwa na kitu butu, na watuhumiwa hao pia walimpora pikipiki yenye namba za usajili MC.464 ELL aina ya Kinglion.

"Baada ya kupata taarifa za mauaji hayo, Polisi tulianza msako mkali na Desemba 3, mwaka huu, huko Mlowo wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, tulifanikiwa kuwakamata watuhumiwa wa mauaji ya mwenyekiti huyo," alisema ACP Siwa.

Alisema waliwakuta watuhumiwa wakiwa na pikipiki ya marehemu Kalinga na kwamba upelelezi wa shauri hilo unaendelea kwa ajili ya hatua zingine za kisheria kuchukuliwa.

Kutokana na tukio hilo, Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya linatoa onyo kwa baadhi ya wananchi ambao wanaendelea kujihusisha na vitendo vya uhalifu kuacha mara moja kwani uhalifu haulipi na badala yake wajihusishe na shughuli halali za kujipatia kipato.

Kwa mujibu wa Anderson kalinga, baba mzazi wa marehemu, mazishi yalifanyika jana katika Kata ya Makongolosi wilayani Chunya.

Mkoani Kilimanjaro, polisi linawashiklia watu watatu kwa tuhuma za mauaji ya Isack Malya (71), aliyeuawa kwa kupigwa na kitu butu kichwani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Simon Maigwa, alisema jana kuwa mauaji hayo yalifanyika Desemba 02, mwaka huu, majira ya 2:00 asubuhi katika kijiji cha Kibosho Umbwe Onana.

Alisema siku ya tukio, Malya akiwa nyumbani kwake, alishambuliwa na watuhumiwa hao, walimshambulia na kumpiga na kitu butu kichwani na kutokomea kusikojulikana.

Kamanda Maigwa alisema polisi kwa kushirikiana na wananchi, walifanya msako na kufanikisha kuwakamata watuhumiwa hao ambao wanaendelea kuhojiwa na taratibu za kisheria zitakapokamilika, watafikishwa mahakamani.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@ guardian.co.tz***

# Waandishi watahadharishwa matumizi akili mnemba

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAANDISHI wa habari nchini wametahadharishwa kuhusu matumizi ya teknolojia ya akili mnemba (AI) kutokana na kuwa sehemu ya upotoshaji.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika Tawi la Tanzania (Misa-Tan), Salome Kitomari, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa kwenye ufunguzi wa mkutano wa taasisi hiyo.

Kitomari aliwataka wanahabari kuchukua tahadhari kuhusu teknolojia hiyo ambayo imewarahisishia wanahabari duniani kupata habari kwa urahisi, lakini sio kila habari inayopatikana huko ni sahihi.

Kadhalika alisema teknolojia hiyo ina matokeo chanya na hasi na kwamba kuna uwezekano wa kuwa habari ya kutengeneza na mwandishi asipofuatilia vizuri atapotosha.

Alitoa mfano wa picha bandia kuwa waandishi wanatakiwa kuchukua hatua ya kuhakiki upande mwingine.

"Upande wa mafanikio teknolojia hiyo imerahisisha upatikanaji wa habari pamoja na kutengeneza vichwa vya habari kwa magazeti na mitandao ya kijamii," alisema.

Aidha, alisema katika mkutano huo kutakuwa na uchaguzi wa kuwapata viongozi wapya wa Taasisi hiyo.

Alizitaja nafasi hizo zitakazogombewa kuwa ni mwenyekiti, makamu mwenyekiti na wajumbe wa tatu wa bodi ya taasisi hiyo.

Mwenyekiti huyo alisema kwa mujibu wa katiba ya taasisi yao watakaochaguliwa wanakaa madarakani kwa muda wa miaka mitatu.

Hata hivyo, alisema kwa mujibu wa katiba hiyo viongozi waliopo wamemaliza muda wao na watakabidhi madaraka baada ya uchaguzi.

Akifungua mkutano huo, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabiri Shekimweri, aliwataka waandishi wa habari kutumia vyanzo sahihi vya habari hasa katika kuelekea kipindi cha uchaguzi mkuu mwakani.

Aidha, aliwataka kujitofautisha na watu wengine wanaotumia mitandao ya kijamii kupotosha umma.

# Askari polisi waachiwa huru kesi unyang'anyi mil. 90/- kutumia silaha

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imewaachia huru askari watatu wa Jeshi la Polisi waliokuwa wanashtakiwa katika kesi ya wizi wa kutumia silaha kumnyang'anya mfanyabiashara Grace Matage Sh. milioni 90.

Askari hao wameachiwa huru baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha dhidi yao.

Waliachiwa huru ni Koplo Ramadhani Tarimo (42) maarufu kama Rasta, Koplo Majid Abdallah (35), Koplo Stella Mashaka (41) mkazi wa Railway. Mbali na askari hao, wengine waliokuwa wanashtakiwa ni Ashraf Sango (31) na Emmanuel Jimmy (31).

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi Franco Kiswaga, alisema jukumu ya kuthibitisha shtaka ni upande wa mashtaka na kwamba katika mashahidi wote saba, hakuna hata mmoja aliyethibitisha kuwa askari hao walifanya unyang'anyi huo.

Alisema washtakiwa wote wanashtakiwa kwa shtaka moja chini ya Kifungu 287 (a) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu na hapo ndipo kwenye msingi wa kesi,. Adhabu yake ni miaka 30 na viboko au bila viboko.

"Ili mahakama imtie hatiani mtu, lazima ioneshe kama kweli nguvu ilitumika katika kufanya wizi. Haya ni uamuzi wa Mahakama ya Rufani yanaelekeza hivi," alisema Hakimu Kiswaga.

Alisema shahidi namba moja, mbili, nne na tano wa upande wa mashtaka walieleza mahakama namna washtakiwa wa kwanza hadi wa tatu (askari polisi) walivyofika ofisini kwake na fedha zilivyochukuliwa. Mwathirika alieleza kwa kirefu alivyokuwa anamtuma mfanyakazi wake kwenda kubalisha Dola za Marekani kuwa Shilingi.

Hakimu Kiswaga alisema tukio hilo lilikuwa si la mara moja kutokana na ushahidi uliotolewa.

"Mahakama inajaribu kujiuliza katika mazingira haya unyang'anyi wa kutumia silaha unawezaje kutumika?"

"Muhanga (mwathirika) katika ushahidi wake alipoulizwa kuwa washtakiwa hao wakati wanachukua fedha hizo walikuwa wamemwoneshea silaha, akadai Hapana. Mahakama inaendelea kujiuliza unyang'anyi wa kutumia silaha unaweza kutumika hapa?," alisema Hakimu Kiswaga

Aidha, alisema mahakama inaendelea kujiuliza kuwa tukio hilo lilitokea Agosti 28,2023 lakini halikuripotiwa siku hiyo kituo cha polisina lililipotiwa mwezi mwingine baadaye, hivyo inawezekanaje kukatokea unyang'anyi huo na mashashidi wote wakakaa kimya.

Pia alisema mahakama inajiuliza kwamba hakuna ushahidi uliofikishwa mbele yake kuwa fedha hizo zilichukuliwa na kupelekwa eneo la Kurasani na pia hakuna uthibitisho kama fedha hizo zilikuwa Dola za Marekani.

# Siri wananchi kutumia mitandao kijamii kufikisha malalamiko serikali hadharani

**Na Lusungu Helela,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Xavier Daudi, amesema wananchi wengi wamekuwa wakitumia mitandao ya kijamii kufikisha malalamiko yao kwenye taasisi za serikali kutokana na baadhi ya watumishi kuvujisha siri pindi wananchi hao wanapotumia mifumo rasmi kutoa mrejesho.

Amesema vitendo hivyo vimekuwa vikiwakatisha tamaa wananchi wenye nia njema ya kuona serikali inakuwa kinara wa kutoa huduma bora kwa wananchi.

Daudi alisema hayo juzi jijini hapa wakati akifungua mafunzo maalum ya siku tatu kwa maofisa mrejesho kuhusu uendeshaji wa mfumo wa e-Mrejesho katika ofisi za umma.

Kutokana na kuwapo tatizo hilo, aliwataka maofisa hao kutunza siri za wateja ili kuwafanya wananchi kuwa huru kuwasilisha changamoto zinazowakabili wakati wowote na mahali popote pasipo kulazimika kutumia mitandao ya kijamii.

Daudi aliongeza kuwa mfumo wa e-Mrejesho unampa fursa mwananchi kutuma malalamiko, pongezi na maulizo kwa serikali mahali popote na wakati wowote.

Naibu katibu Mkuu aliwataka maafisa hao baada ya kurudi katika vituo vyao vya kazi, wakahakikishe wanakuwa waadilifu kwa kutunza siri za ofisi na za wateja ili kuwafanya wananchi kuwasilisha malalamiko yao kwenye njia rasmi.

Pia aliwataka maafisa hao wakaimarishe madawati au ofisi za mrejesho zilizoko katika taasisi zao ili kufanikisha ushughulikiaji mrejesho kwa ufanisi na kwa wakati katika ofisi za umma kwa vile wameaminiwa kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi.

Mkurugenzi wa Usimamizi wa Utawala Bora kutoka USAID/PS3+ awamu ya pili, Dk. Emmanuel Malangalila, alisema wataendelea kushirikiana na serikali ya Tanzania katika kuhakikisha mfumo huo unatumika ipasavyo katika serikali za mitaa ambako ndiko kuna malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi.

"Mafunzo haya yanalenga kuona huduma zinazotolewa na serikali zinafurahiwa na wananchi wote bila kujali rangi, kabila, mahali au hali zao za kiuchumi,' alisisitiza Dk. Malangalila.

Hivi karibuni, Tanzania ilipewa tuzo ya Kimataifa ya ubunifu wa mfumo ya kidijitali wa Mrejesho (e-Mrejesho) nchini Korea Kusini na Umoja wa Mataifa (UN) wakati wa Mkutano wa Umoja wa Jukwaa la Umoja wa Mataifa la Tuzo za Utumishi wa Umma (2024 UN Public Service Awards (UNPSF) kutokana na umadhubuti wake.





COOKFUND
clean cooking solutions

Accelerated Market roll-out of Clean Cooking Solutions in Tanzania

**INNOVATION CHALLENGE FOR CLEAN COOKING**

**Call for Applications**

**Summary**
The CookFund programme is a five-year (2021 – 2026) programme established by the Government of Tanzania (through the Ministry of Energy) in collaboration with the European Union (EU) and implemented by UNCDF. The programme aims to contribute to Tanzania's climate change commitment by increasing the share of the population with access to sustainable cooking solutions. The CookFund provides catalytic grant funds to private enterprises to address the affordability challenges that hinders the accelerated use of clean cooking solutions in households. The clean cooking solutions supported by the programme include LPG, electric pressure cookers, bioethanol, improved charcoal stoves and briquettes. The programme is focused on five regions of mainland Tanzania, namely, Dar es Salam, Mwanza, Dodoma, Morogoro and Pwani.

**The Call for Applications**
UNCDF is inviting interested and eligible individuals and companies from across Tanzania involved in the clean cooking value chain to submit applications to the CookFund Innovations Challenge. The challenge targets **innovative solutions** in stove and fuel technology, cooking products financing and behavioural change approaches with the potential to accelerate the acceptance and use of clean cooking in Tanzania. Youth and women innovators are **encouraged** to apply. Special consideration will be provided to youth and women applications.

**Application:** For the detailed Call for Applications Guidelines (including the eligibility criteria) and Application Form, please visit **https://uncdf.link/innchallenge.**

**Language:** All application forms must be submitted in English.

**Deadline for submission:** This application is open from 25th November 2024 to 15th December 2024.

**Pre-submission info session:** UNCDF will conduct an online pre-submission info session to provide guidance on how to prepare applications, increase the understanding on submission requirements and offer applicants an opportunity to raise questions. If you wish to participate, please send an email to **cookfund.tz@uncdf.org** indicating *"Innovations Challenge Pre-submission Info Session"* in the subject line of your email. The specific date and time for the workshop will be communicated to those who will request participation.

Please note that participation to the online pre-submission info session is not a prerequisite for responding to this call.

For further information and/or questions, please contact:
UNCDF Tanzania, Email: **cookfund.tz@uncdf.org**
Tel: +255 22 260 0911

MINISTRY OF ENERGY | UN CDF Impact Capital for Development | UNIDO | Funded by the European Union

182823

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Uamuzi wa stempu maalumu TRA umefanyika kwa wakati mwafaka*

**MAMLAKA** ya Mapato Tanzania (TRA) imekuwa ikiongeza juhudi mbalimbali katika ukusanyaji wa mapato yanayotokana na kodi yakiwamo kodi ya mapato, ushuru wa bidhaa na forodha. Jitihada hizo zimezaa matunda na mamlaka hiyo imekuwa ikitoa taarifa za kuongezeka kwa mapato mara kwa mara.

Katika taarifa iliyotolewa juzi na Kamishna Mkuu wa TRA, Yussuf Mwenda, kwa mfano, mamlaka imekusanya Sh. trilioni 12.33 kuanzia Julai hadi Novemba, mwaka huu. Makusanyo hayo ni zaidi ya lengo lililokuwa limewekwa katika kipindi hicho ambalo ni Sh. trilioni 12.30. Ongezeko la makusanyo hayo yanadhihirisha kuwa mamlaka hiyo imeweka mikakati thabiti kuhakikisha malengo yanatimiza na hata kuvuka. Hatua hiyo inatoa matumaini kwamba serikali inaweza kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na matumizi ya ofisi kama vile kulipa watumishi mishahara na stahiki zao.

Pamoja na jitihada hizo, TRA imekuwa ikikumbana na vikwazo mbalimbali ambavyo vinarudisha nyuma jitihada zake katika kutimiza hayo. Miongoni mwa vikwazo hivyo ni baadhi ya wafanyabiashara kushirikiana na watumishi wasio waaminifu kukwepa kodi, makadirio yasiyo sahihi kwa wafanyabiashara, baadhi ya wafanyabiashara kutotumia mashine za risiti za kielektroniki (EFD) na kuingizwa sokoni kwa baadhi ya bidhaa bila kulipiwa kodi au kutokuwa na stempu zinazotambuliwa na mamlaka.

Kutokana na kubaini uwapo wa baadhi ya bidhaa sokoni ambazo hazina stempu za kielektroniki (ETS), hasa vinywaji vikali, TRA imetengeneza stempu maalumu kwa ajili ya kudhibiti pombe feki sokoni. Kwa mujibu wa Kamishna Mkuu Mwenda, stempu hizo zenye alama nyingi za ulinzi na mwarobaini katika bidhaa bandia sokoni, hasa vinywaji.

Kwa mujibu wa Kamishna Mkuu, stempu hizo si rahisi kuzinakili na kwamba uwapo wake utasaidia kuongeza mapato na kupunguza tatizo la bidhaa feki hasa pombe sokoni ambazo kwa sasa zinauzwa kama njugu hata kwenye vituo vya mabasi ya abiria, maarufu kama daladala kwenye miji mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha, Dodoma na Mwanza.

Sambamba na kuwapo kwa stempu hizo, TRA pia inaendelea kutoa elimu na kufuatilia kwa wafanyabiashara wasiotumia stempu sahihi ili wale wanaobainika kukiuka matumizi hayo wachukuliwe hatua za kisheria.

Kwa hakika mpango uliobuniwa na TRA kuwa na stempu maalumu ambazo zitawabana wafanyabiashara wanaouza bidhaa bandia sokoni ni cha kupongezwa. Mpango huo si kwamba tu utasaidia kudhibiti ukwepaji kodi na kuongeza mapato bali pia utasaidia kuokoa afya za watumiaji wa vileo vikali kutokana na pombe au bidhaa wanazotumia kutokuwa na uhakika wa usalama kwa afya zao.

Hivi sasa katika maeneo mbalimbali kumeibuka wimbi kubwa la biashara ya pombe kali ambazo baadhi zinauzwa kwa bei rahisi na watumiaji wake ambao ni vijana wamekuwa wakiathirika kiafya. Vijana hao ni rahisi kuwakuta kwenye vituo vya mabasi wakiwa wamelewa chakali na hawawezi kufanya kazi yoyote ya uzalishaji.

Licha ya kuwapo sokoni kwa bidhaa hizo, jitihada zingine za TRA kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, zinapaswa kuelekezwa katika msako wa maeneo ambako pombe hizo zinatengenezwa ili kudhibiti kuingiza kwa bidhaa hizo bandia kwenye soko.

Swali la kujiuliza iweje wamiliki wa viwanda wanaolipa kodi za mabilioni ya shilingi taswira yao iharibiwe na watu wachache wanaotengeneza pombe zisizo na viwango? Watu hao wenye viwanda bubu vya kutengeneza pombe feki hawana budi kukamatwa na kuchukuliwa hatua stahili.

Aidha, ndani ya TRA kuna baadhi ya watumishi wanaotuhumiwa kushirikiana na wafanyabiashara kukwepa kodi na inawezekana wanasaidia kutoa stempu feki kwa manufaa yao binafsi. TRA inapaswa kuliangalia hilo kama waswahili wasemavyo kusafisha nyumba yako ndipo uende kwa jirani. Watu hao wasipewe nafasi hata kidogo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# *Mabinti kujitunza ni wajibu wa msingi, jiangalieni vyema!*

Na Joyce Lameck

**LICHA** ya kuwafunza mabinti zetu jinsi ya kujitunza ili wasipate mimba za utotoni na zisizotarajiwa, bado kuna wajibu tunapaswa kuwaambia ukweli kuhusu madhara ya utoaji mimba usio salama.

Hiyo ni kwa sababu, kuna idadi kubwa ya mabinti wanaokumbana na changamoto ya mimba zisizotarajiwa, ikianzia kwenye ukatili kingono, kubakwa na maharimu, wanaishia kuzitoa kwa njia zisizo salama.

Japo kutopatikana taarifa kamili za mimba zinazotokana na matukio ya ukatili wa kijinsia, ikiwamo unyanyasaji wa kingono, ubakaji na kuwepo kwa mimba zisizotarajiwa.

Bado kuna idadi kubwa ya matukio kama haya, ambayo hurekodiwa katika vituo vya polisi vilivyowekwa maalum, kwa ajili ya jinsia katika mikoa mbalimbali nchini, kutokana na utafiti uliofanywa wa sensa ya afya na malaria, utafiti uliofanywa na TDHS, 2022.

Wazazi wengi wamekuwa wakiwaeleza mabinti zao, namna wanapaswa kuchukua tafadhali kujilinda juu ya masuala ya kupata mimba katika umri mdogo na pindi wanapokuwa shuleni, ili kuweza kuhitimu masomo yao.

> **Wazazi wengi wamekuwa wakiwaeleza mabinti zao, namna wanapaswa kuchukua tafadhali kujilinda juu ya masuala ya kupata mimba katika umri mdogo na pindi wanapokuwa shuleni, ili kuweza kuhitimu masomo yao.**

Tukiachilia mbali masuala ya elimu hiyo bado wanahitaji kuelezwa kuwa utoaji mimba kiholela ni hatari kwa afya zao na wanaweza kupata madhara makubwa ambayo yataleta majuto maisha yao yote.

Tukumbuke kuwa mabinti wote hupata mimba zisizo tarajiwa kwa kutaka, kuzitafuta, lahasha! Walio wengi hupata mimba hizo kwa ukatili wa kingono, kubakwa na kupitia mahalimu (ndugu wa karibu). Na kwa kuogopa sheria na maadili ya nchi yetu, huishia kujificha kwa wazazi, walezi kwa kuhofia hivyo, huishia kupata ushauri usio sahihi na kwenda kutoa kwa kutumia njia zisizo sahihi na zenye madhara.

Madhara hayo yanaweza kuwa ni ya muda mfupi au mrefu, pia kukosekana kwa wingo mpana wa utoaji mimba kisheria na usalama hasa kwa mimba zitokanazo na matukio hayo matatu, kumeathiri sana afya ya kimwili na kiakili ya mabinti walio wengi nchini.

Utafiti wa matabibu unaonesha waathirika wa mimba zisizotarajiwa wanaweza kuathirika kisaikolojia, kiafya na hata kijamii na kuwa athari hizo zinaweza kuwa za haraka na kudumu zikiathiri maeneo mbalimbali ya maisha.

Vilevile changamoto ya kupata mimba katika umri mdogo una madhara, lakini madhara makubwa zaidi hutokea pale zinapotumiaka njia za mafichoni au vichochoroni katika kutoa mimba. Hivyo kama wazazi na walimu tutawaeleza ukweli mabinti zetu kuhusu madhara ya utoaji mimba usio salama na kuwa ni vema inapotokea hilo ni vema kuwaona wataalamu ili kuweza kuwasaidia.

Hata hivyo, kwa sasa mambo yamebadirika si kama zamani kuwa, unapogundulika umetoa mimba kwa kutumia njia za vichochoroni, huwezi kusaidiwa na wataalam wa afya, kwa sababu ya sheria.

Sasa imekuwa tofauti kwasababu mwanamke, binti anapokuwa ametoa mimba kwa njia zisizo salama, bado anatakiwa kwenda hospitali ili kupatiwa matibabu sahihi na kupatiwa elimu juu ya uzazi salama.

Huduma hii inapatikana katika vituo vya afya na hata katika hospitali za serikali, tena bila gharama yoyote kwa matibabu hayo, kupatiwa ushauri na kupimwa magonjwa kama vile VVU na saratani ya shingo ya kizazi.

Pia, wataalamu watakupatia ushauri, maelekezo sahihi juu ya uzazi wa mpango, ili usipate tena mimba isiyotarajiwa hadi pale utakapo amua kupata mtoto kwa wakati unaostahili.

Hivyo, basi maboresho ya sheria yatasaidia kupunguza vifo, vitokanavyo na uzazi kwa wanawake na mabinti wengi kwani naamini kama sheria inatazama mazingira ya upatikanaji wa mimba kwa mtu. Naamini maboresho hayo yataleta matokeo chanya, kwani wanawake pamoja na mabinti wamepoteza maisha kwa kutoa mimba zisizotarajiwa, kwa njia zisizo salama na kuishia kupoteza kizazi na wengine kupoteza maisha kabisa.

TANGAZO

# Bonite yang'ara tuzo za Rais za mzalishaji bora viwandani

Kampuni ya Bonite Bottlers iliweka rekodi nyingine baada ya kushinda tuzo ya Rais ya mzalishaji bora viwandani.

Kampuni hiyo imefanikiwa kupata tuzo za Rais za Mzalishaji Bora Viwanda ikishinda katika kipengele cha mzalishaji bora wa vinywaji visivyo na kilevi nchini.

Kampuni ya Bonite Bottlers imeendelea kuzalisha bidhaa zake katika ubora wa hali ya juu, kudumisha ufanisi katika kuwahudumia wateja wake ili kukidhi matarajio ya wateja wake nchini.

Bonite Bottlers, inajihusisha katika uzalishaji wa vinywaji wa bidhaa za Coca-Cola, Maji ya Kilimanjaro, na vinywaji vingine visivyo na kilevi. Akizungumza na gazeti la Nipashe , Mkuu wa Mauzo na Masoko wa Bonite Bottlers, Christopher Loiruk, alisema kuwa tuzo hiyo imeonyesha jinsi kampuni hiyo ilivyofanikiwa kuhakikisha inakidhi matarajio ya wateja kwa kuendelea kuzalisha bidhaa za hali ya juu na kutoa huduma bora kwa wateja wake.

Loiruk alisema mafanikio ya Bonite Bottlers katika tuzo ya PMAYA pia yameonyesha mchango wake mkubwa katika uchumi wa Tanzania na kuwa mfano katika kuwekeza katika ubora wa bidhaa na teknolojia za kisasa.







Aliongeza kuwa siri mojawapo ya ushindi wa tuzo hiyo ni kuzalisha bidhaa zenye ubora wa hali ya juu zinazozingatia viwango vya kitaifa na kimataifa, pamoja na kuwekeza katika teknolojia ya kisasa.

Pia alisema kuwa kampuni ya Bonite Bottlers imeweza kujitofautisha sokoni kupitia bidhaa mbalimbali inazozalisha huku ikidumisha uhusiano wa karibu na wateja wake kupitia wawakilishi waliofunzwa katika nyanja mbalimbali.

Loiruk alisema kuwa tuzo ya PMAYA ina maana kubwa kwa kampuni ya Bonite Bottlers kwani inaonyesha jinsi wateja kote nchini na Afrika Mashariki wanavyoiamini bidhaa zake.

"Ushindi huu ni chachu kampuni yetu ya kuendelea kuhakikisha kila bidhaa tunayozalisha inakidhi viwango vya ubora vinavyotakiwa. Lengo letu kuu ni kuwapatia watumiaji bidhaa bora na kwa wakati." alifafanua.

Aidha, alisema kuwa hii ni mara ya tatu kwa Bonite Bottlers kushinda tuzo ya PMAYA, ambapo mafanikio yake yanatokana na kuzalisha bidhaa bora kutoka vyanzo asili vya kipekee, jambo linaloimarisha imani kwa wateja wake.

Aliongeza kuwa, katika kukabiliana na changamoto ya bidhaa bandia, kampuni ya Bonite Bottlers ina mtandao mkubwa wa wasambazaji na mawakala nchi nzima, ambao huwasaidia kutambua na kushughulikia haraka masuala yoyote yanayohusiana na bidhaa zake.

"Kwa kufanya hivyo, kwanza tunahakikisha mchakato wetu wa uzalishaji hauleti nafasi ya kughushi kwa kuingiza vipengele vya kiusalama katika bidhaa zetu. Pili, tuna ufuatiliaji wa karibu kupitia wafanyakazi wa kampuni katika maeneo ya biashara ili mara kwa mara kuhakiki bidhaa zinazouzwa. Pia jamii yetu inapaswa kufichua yeyote anayehusika na kusambaza taarifa potofu kuhusu kampuni na bidhaa zetu ili wachukuliwe hatua za kisheria wale wanaoghushi," aliongeza Loiruk.

Hata hivyo, alisema kuwa mbali na kushinda tuzo hiyo, mafanikio mengine ambayo Bonite Bottlers inajivunia ni kuwa moja ya kampuni zinazoshirikiana kwa karibu na jamii ya kitanzania, ikidhamini matukio mbalimbali ya kijamii kama vile michezo na burudani, na pia kushiriki kusaidia jamii katika nyakati za changamoto mbalimbali.

Tuzo za PMAYA za 18 zilifanyika jijini Dar es Salaam Novemba 8 ambapo mgeni rasmi alikuwa Dk. Philip Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

PMAYA imeandaliwa na Shirikisho la Viwanda Tanzania (CTI) kwa kushirikiana na wadau wengine kwa lengo la kutambua juhudi za wazalishaji wa ndani wanaochangia uchumi wa taifa kwa kuzalisha bidhaa za hali ya juu wa ndani na nje ya nchi.

218285202







kilimanjaro_drinking_water kilimanjarodrinkingwater kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

# TANGAZO

## NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD,JAMOK INVESTMENT LTD,MCHINGA AUCTION MART,GADAU AUCTION MART,AMI AUCTION MART, IGALULA AUCTION MART,BAHARI AUCTION MART, ADILI AUCTION MART,KOTI BROTHERS CO. LTD,PROPERTY MASTER LTD,MULTILINK AGENCY LTD,TWINS AUCTIONS MART, BID CITY AUCTION,JALAS AUCTION MART,HOLLYNESS COMPANY LTD kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.**

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| UKONGA | WAWA COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.KND/KGG/KATI/214 KIGOGO KATI 2. NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOPO KINZUDI GOBA | 1.SALUM JUMA MARWA 2.SALUMU JUMA NYANDOTO | 1.KIGOGO KATI 2.KINZUDI GOBA | 13/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | NEZAK INVESTMENT LTD | NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1019002 KIWANJA NAMBA P23439 KIFURU-KINYEREZI | ZACHARIA ANTHONY KAPAMA | KIFURU KINYEREZI-ILALA | 12/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | TEMSO ENGINEERING AND CONSTRUCTION CO. LTD | NYUMBA YENYE HATI NA.58326,KIWANJA NA.2000,KITALU 'A' | RAYMOND LUDOVICK TENGA | PUGU KAJIUNGENI | 10/12//2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KARIAKOO | MBM MOTORCYCLE SPARES | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NAMBA 101, KITALU "47", HATI NAMBA 52425 | PETER SIMON MSANZYA | KIJITONYAMA -DAR ES SALAAM | 12/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | PETER JAPHET CHAMBA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK013453 | KELVIN DAVID CHAMBA | YOMBO VITUKA SIGARA TEMEKE | 11/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 12/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | TUNDUMA | 10/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | KITETE-MBEYA | 10/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 11/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA ( 2) | 1.FRENK SAMSON LEMAU 2.MARIAM PETER NGAJILO | 1.SHEWA-MBEYA 2.ITUHA MBEYA | 12/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | IPYANA TIGER JUNIOR | NYUMBA | IPYANA TIGER JUNIOR | ILEMI | 13/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | WILLY MWITIKA MGOGO | NYUMBA | WILLY MWITIKA MGOGO | MLOWO | 16/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FELIX MAVIKE MSIGWA | NYUMBA | FELIX MAVIKE MSIGWA | ILEMI | 13/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | KEVINI MONDELO TAVE | NYUMBA | KEVINI MONDELO TAVE | ILEMI | 19/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | CHARLES JOHN ZIMBA | NYUMBA | CHARLES JOHN ZIMBA | ITEZI -MASHARIKI | 17/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | KUMBUSO MSAKAFU NGOGO | NYUMBA | KUMBUSO MSAKAFU NGOGO | MBUYUNI RUJEWA MBARALI | 19/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | LAMECK JOHN RUGIGA | NYUMBA | LAMECK JOHN RUGIGA | KIBAMBA MBEZI | 13/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | SULTAN MSHINDO KATUNDU | NYUMBA | SULTANI M.KATUNDU | KIMANZICHANA | 12/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | TRAZIAS BERNARD ISHENGOMA | KIWANJA | TRAZIAS BERNARD ISHENGOMA | MBAGALA MWANAMTOTI | 06/12/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HOSEA MARCO OOKO | NYUMBA | KIBADENI J. NYATIENO | ZAVARA -ILALA | 13/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | DAUDI JAKAMUGAH MAKOSIGAH | NYUMBA | KIBADENI J. NYATIENO | ZAVARA -ILALA | 13/12/2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | ATUPELE LABAN MWAIJIBE | NYUMBA | DR. ATUPELE LABAN MWAIJIBE | KIPUNGUNI | 17/12/2024 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | FELIX BIRCKMAS ALOYS | NYUMBA | KASSIAN ANTHON NINDI | TABATA KISUKULU | 18/12/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ILALA | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK033735 | DAVID ABEL MLAU | CHARAMBE -MBAGALA | 11/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | NELSON JUDICA KIMARO | NYUMBA (2) | 1.NELSON JUDICA KIMARO 2.ERICK ISHENGOMA BILIKWIJA | 1.KIMARA BONYOKWA 2.MABIBO | 16/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | JESCA PETER SHIRIMA | NYUMBA | JESCA PETER SHIRIMA | MJOHORONI MOSHI | 13/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | CHEGE REUBEN OGILLO | NYUMBA | CHEGE REUBEN OGILLO | MSARANGA MOSHI | 13/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | MWAJABU AHMEDI KIBWANA | NYUMBA | MWAJABU AHMEDI KIBWANA | BOMANG'OMBE HAI | 12/12/2024 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | JUMA SELEMANI MNDEME | NYUMBA | JUMA SELEMANI MNDEME | MWANGA | 16/12//2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | PLUKERIA MARTIN MANINGI | NYUMBA | PLUKERIA MARTIN MANINGI | KIBOSHO -KOMBO | 13/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | SAMIJI ATHUMANI KIMBWEREZA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | SAMIJI ATHUMANI KIMBWEREZA | MAKANYA SAME | 16/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | MOSES YARED CRY | NYUMBA | MOSES YARED CRY | ZAVARA BUYUNI | 10/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | RAYMOND SAMSON LAISER | NYUMBA | RAYMOND SAMSON LAISER | KIHARAKA BAGAMOYO | 17/12/2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | MTIBU FISH ENTERPRISES | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.DSMT1026616, BONYOKWA | HAMISA BAUSI ABUU | KIMARA BONYOKWA | 17/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ILALA | LAURENCIA ROBERT KIROBI | NYUMBA | LAURENCIA ROBERT KIROBI | KIBADA | 10/12//2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ILALA | DANIEL FADHIL MINJA | NYUMBA | DANIEL FADHIL MINJA | MAJOHE | 12/12/2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ILALA | RENIFRIDA CHARLES MGUDE | NYUMBA | RENIFRIDA CHARLES MGUDE | SARANGA | 12/12/2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARIA JOHN PETRO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JOHN PETRO KALISA | KILOLELI 'B' - MWANZA | 12/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO0 |
| MWANZA | MASHAKA CHARLES BULUBA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | MASHAKA CHARLES BULUBA | NYASAKA | 12/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | GRACE ADONIAS MTEGO | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.22 KITALU 'N' HATI NA.4870 | BLASIUS SWAI KAGINA | BUNDA | 13/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | ABAS HAMAD ISSA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PETER NDULU MAHARAGE | MISUNGWI | 16/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JAMES JACOB KALULEMA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JAMES JACOB KALULEMA | NYANGURUGURU MAHINA | 11/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | KITU MAYALA MANGA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | KITU MAYALA MANGA | KISESA | 16/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MAWAZO JOHN SIMON | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | EDWIN GASPARY NYAMTABA | KANYERERE | 16/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JOSIAH JOHN JOACHIM | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JOSIAH JOHN JOACHIM | KISESA MWANZA | 16/12/204 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | CHACHA ITEMBE NYAMAISA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | SHABANI S. BULILO | NYAMHONGOLO | 12/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | HELENA IGNATUS NYAKARASHI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | GEORGE SILIVESTER ADOGO | NYAMADOKE BUSWERU | 17/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MAGWE EMMAUEL WAMBURA | VIWANJA (3) VYENYE HATI MILIKI | MAGWE EMMANUEL WAMBURA | ILALILA-MWANZA | 17/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | IMORY FREDRICK IMORY | NYUMBA,YENYE HATI NA.99386 | IMORY FREDRICK IMORY | BUKAGA MWANZA | 19/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | DENIS DEOGRATIAS NSHEKANABO | NYUMBA YENYE HATI NA.103641,KIWANJA NA.211 | DANIEL MABULA KAHUNGWA | NYAMANORO ILEMEALA | 18/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | ALOYCE ALOYCE KIMARO | NYUMBA | YAHAYA HUSSEIN ATHUMAN | PASIANSI MWANZA | 18/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | HAPPINESS NYANDA MAYALA | NYUMBA YENYE HATI NA. 99009, KIWANJA NA."9" KITALU " F" | SAIDI NYANDA MAYALA | IGOMA MWANZA | 17/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | ABDALLAH AHMAD MUHIDINI | NYUMBA | ABDALLAH AHMAD MUHIDINI | TEGETA 'A' - GOBA | 12/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | MARTHA ONESPHORY NCHIMBI | NYUMBA | MARTHA ONESPHORY NCHIMBI | MGEULE JUU-CHANIKA | 13/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | DEVOTA JOHN KATINDASA | NYUMBA | MASOUD HAMAD SEIF | KICHANGANI- MAJOHE | 12/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | STEWART EDSON MWANGALABA | SHAMBA | STEWART EDSON MWANGALABA | MKURANGA | 18/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | AMRI BAKARI MAKANYA | NYUMBA | MWANAHAMISI KASSIM YUSUPH | KITUNDA | 13/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | JACQUELINE LAMECK KIBOGA | NYUMBA | SABATO DAVID OKUKU | MIKWAMBE- TOANGOMA | 16/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | CESILIA SAMWELY KWEKA | NYUMBA | LEONARD JACOB NUBWA | MBAGALA- MISSION | 19/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | MTUMWA SALUM HAMAD | NYUMBA | MATONGO NKWABI NSWAGA | PUGU KINYAMWEZI | 18/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | ANDREW SAMSON GESURURA | NYUMBA | ANDREW SAMSON GESURURA | BASIHAYA-BOKO | 18/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | MUSSA INANO CHACHA | NYUMBA | HABIBU MUSSA MACHOROKO | MBAGALA | 19/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | SAINT PIO DAY CARE CENTRE | NYUMBA | JESCA JAMES SUGWEJO | MABWEPANDE | 18/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | MWANAHAMIS VITUS FRANK | NYUMBA | HADIJA MOHAMED CHANDE | MSINGWA-MSIGANI | 11/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | SELEMANI HEMED SELEMANI | NYUMBA | SELEMANI HEMED SELEMANI | MBAGALA KIBONDE MAJI | 13/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | SHAMSI FADHILI MASISA | NYUMBA | SAAD ADAM MDOE | KINYAMWEZI KATA YA PUGU | 16/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | WINNIE ADOLE RWIZA | NYUMBA | WINNIE ADOLE RWIZA | KANGA-KINYEREZI | 11/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | SALVATORY MODESTI NGOWI | NYUMBA | SALVATORY MODESTI NGOWI | KIPUNGUNI 'B'-KITUNDA | 12/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | FREDRICK ALLY SANGA | NYUMBA | FREDRICK ALLY SANGA | KIVULE-ILALA | 13/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | FATUMA MSOMA KIULA | NYUMBA | AMIRI OMARI LUPATU | MAJOHE-KICHANGANI | 18/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | JIMMY MLAGANO CHANGAS | NYUMBA | JIMMY MLAGANO CHANGAS | BUNJU "B" | 16/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | GIDION YORAM ISACK | NYUMBA | GIDION YORAM ISACK | CHANIKA-YONGWE | 17/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | LEOKADIA SOSTHENES MPONZI | NYUMBA | LEOKADIA SOSTHENES MPONZI | MACHIMBO - KIPUNGUNI | 18/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | GLADNESS PETER BOLOHO | NYUMBA | GLADNESS PETER BOLOHO | BOMBAMBILI KIVULE | 13/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | ONESMO PETER MASIMA | NYUMBA | ONESMO PETER MASIMA | UKONGA MAZIZINI | 13/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | JULIUS RYOBA DANIEL | NYUMBA | JULIUS RYOBA DANIEL | KITUNDA- MZINGA, ILALA | 16/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | MAX AYUBU MBONYE | NYUMBA | MAX AYUBU MBONYE | YONGWE-CHANIKA | 18/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | ROBERT CHACHA NYAMBARI | NYUMBA | ROBERT CHACHA NYAMBARI | KITUNDA MTAA WA KINYANTIRA | 11/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | ABDALLAH SEIF MATIMBWA | NYUMBA | ABDALLAH SEIF MATIMBWA | VIWEGE-MAJOHE, ILALA | 11/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | AMA ABDALLAH KIPENDE | NYUMBA | AMA ABDALLAH KIPENDE | KIBAONI KISARAWE - PWANI | 17/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | CHRISTOPHER CHACHA MAGWE | NYUMBA (2) | 1. CHRISTOPHER CHACHA MAGWE 2. EUNICE ELIGUARD MMARI | 1.CHINANGALI 2.NALA - DODOMA | 17/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | IVAN MAWAZO JACKSON | NYUMBA | IVAN MAWAZO JACKSON | MPUNGUZI -DODOMA | 13/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ARUSHA | OLIVER STANLEY MNDEME | NYUMBA | OLIVER STANLEY MNDEME | KIMANDOLU - ARUSHA | 11/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MAIN | JAR TECHNOLOGIES | NYUMBA | JULIANA EPIMARK MBWANI | UNGINDONI KIBAHA | 11/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | JAMAL SWALEHE RASHID | NYUMBA | JAMAL SWALEHE RASHID | NALA-DODOMA | 13/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | ROBERT NASSON MAKAPI | NYUMBA | ROBERT NASSON MAKAPI | HOMBOLO BWAWANI - DODOMA | 20/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | KOLE JOSEPH SAINI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | KOLE JOSEPH SAINI | BOMBAMBILI ILALA DAR ES SALAAM | 16/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | CHRISTOPHER MOSSES MWEMA | NYUMBA | CHRISTOPHER MOSSES MWEMA | NZUGUNI ' C' DODOMA | 18/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | CHRISTINA MAGOTI KANGOYE | NYUMBA | CHRISTINA MAGOTI KANGOYE | MSALATO DODOMA | 19/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | JUMBE MHINA SALUM | NYUMBA | JUMBE MHINA SALUM | MKENGE-VIKAWE | 13/12/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | SYLIVESTER APOLINARY MBOYA | NYUMBA (2) | 1. SYLIVESTER APOLINARY MBOYA 2.KIMANGARE BAKARI NJAMA | 1.MBEZI MSUMI 2.ZOMBOKO CHARAMBE | 17/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | MPOKI BROWN MWAIPASI | NYUMBA | MPOKI BROWN MWAIPASI | KILUVYA | 17/12/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | YOHANA MICHAEL NGOIMA | NYUMBA | YOHANA MICHAEL NGOIMA | CHANIKA | 19/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | MARGRETH MTEI MWAISAKA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | MAGRETH MTEI MWAISAKA NA MASHAKA MWAISAKA | KIMARA | 19/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | RAPHAEL BONIVENTURE MMANDA | NYUMBA | BENEDICT MWITA ROBERT | IGOMA - MWANZA | 19/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | NEW FATHER BOLT GENERAL SUPPLIES | NYUMBA | ABDALLAH SULTANI MATOPE | MBAGALA CHARAMBE | 11/12/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu **no.0714939933/0759648448/0715868000/0714208208/0759648448/0755337777/0715363537/0713306054**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

## TANGAZO

**MAJEMBE AUCTION MART KWA MAMLAKA TULIYOPEWA NA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA CHINI YA AKIBA COMMERCIAL BANK PLC Tutauza Magari ambayo ni mali ya Benki hiyo kwa njia ya Mnada.Taarifa za gari na tarehe ya Mnada huo kama inavyojieleza hapo chini**

| JINA LA MMILIKI | NAMBA YA GARI | AINA YA GARI | MAHALI GARI ILIPO | MWAKA WA KUTENGENEZWA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| AKIBA COMMERCIAL BANK LIMITED | T973 AYF | TOYOTA HILUX PICK-UP | AKIBA BENKI HEAD OFFICE | 2008 | 13/12/2024 SAA 4:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AKIBA COMMERCIAL BANK PLC | T749 DKJ | NISSAN HARDBODY PICK-UP | AKIBA BENKI HEAD OFFICE | 2016 | |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Gari ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu **No.0715868000/0754301930**

182851



# Wanaharakati wapiga kambi Moshi Vijijini

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WANAHARAKATI 32 wa Jukwaa la Ukombozi wa Mwanamke Kimapinduzi (TAPO) na Shirika la kiraia la KWIECO, wameanza kuwajengea uwezo wanafunzi wa shule shikizi za msingi Azimio na Papiliki zilizoko Moshi Vijijini mkoani Kilimanjaro kukabiliana na ukatili wa kingono kuanzia majumbani hadi shuleni.

Katika kongamano la elimu ya ukatili lililofanyika viwanja vya shule hizo katika Kijiji cha Uchira, Kata ya Kirua Vunjo Kusini, mmoja wa wanafunzi (jina limehifadhiwa), aliwaeleza wanaharakati hao alivyoshuhudia mwenzake aliyekuwa akiishi naye nyumba moja, alivyopoteza ndoto yake ya kupata elimu baada ya kubakwa nyumbani kwao.

Akizungumza jana, wakati wa kutoa elimu hiyo katika Siku 16 za Uanaharakati Kupinga Ukatili, Mratibu wa Mradi wa Sauti ya Haki, unaotekelezwa na KWIECO kwa ufadhiliwa na Women Fund Tanzania Trust (WFT), Veronica Ollomi, alisema ukatili wa kingono ni tendo lolote la kingono, kama vile kugusa, kubusu, kusugua au kujamiana bila idhini.

"Hii inamaanisha kwa mwathirika hakukubali kufanya hivyo na alilazimishwa, alidanganywa au kuendeshwa kufanya.

Haijali kama tendo lilikamilishwa au lilijaribiwa tu. Ndio maana katika siku hizi 16 za kupinga ukatili tumeamua kuja kutoa elimu kwa wanafunzi wa shule hizi ili kujenga uelewa kwao na kukataa vitendo hivi," alisema.

**Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Papiliki, Halima Mtei alisema: "Kweli tuna kila namna ya kuwashukuru wanaharakati kwa kuja hapa shuleni na kuwapatia watoto...**

Mmoja wa wanafunzi hao, alieleza namna wanavyochukizwa na matukio ya ukatili wa kingono, hasa ubakaji na ulawiti yanavyojitokeza kila uchao, licha ya adhabu kali zinazotolewa na mahakama.

Alisema yeye ni miongoni mwa watoto aliyeshuhudia mwenzake aliyekuwa akiishi naye alivyopoteza ndoto yake baada ya kubakwa nyumbani kwao.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Papiliki, Halima Mtei alisema: "Kweli tuna kila namna ya kuwashukuru wanaharakati kwa kuja hapa shuleni na kuwapatia watoto elimu kuhusu ukatili wa kijinsia.

"Ninaamini kwa kweli tumelipokea kwa furaha sana, kwa sababu naamini watoto walichokipata kitawajenga na kitabadilisha mtazamo wao wakiwa nyumbani, wakiwa shuleni."

Elizabeth Kavishe, Mkuu wa Shule ya Msingi Azimio, alisema anawashukuru wanaharakati hao na KWIECO kuwaelimisha wanafunzi wa shule yake kuhusu ukatili wa kijinsia.

Jenifa Kassim, Mwenyekiti wa TAPO, Moshi Vijijini, alisema: "Tumeamua kutembelea shule za msingi Azimio na Papiliki kuwapa elimu wanafunzi kuanzia darasa la kwanza mpaka la saba tumefanikiwa sana kuwapa pia elimu walimu, ninaamini kupitia hilo watoto wetu watakuwa wameelimika."

Aliongeza: "Pia Ninawashukuru wanaharakati 32 wanaofanya kazi hii katika Kata ya Kirua Vunjo Kusini, ambayo ina vijiji sita na hapa wapo leo wote."



Mkuu wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Kaslida Mgeni (wa pili kushoto), akikata utepe kuzindua kambi ya matibabu ya magonjwa yasiyoambukizwa, yaliyoandaliwa na kampuni ya Mtabe Group kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa wilaya, katika Kituo cha Afya Hedaru, juzi. Kulia ni Mkurugezi Mtendaji wa kampuni hiyo, Jerald Agrey na (kushoto) ni Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Alex Alexander. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Afya ya uzazi kuimarishwa kwa wanawake, wenye ulemavu

**Na Oscar Assenga,** TANGA

SHIRIKA la Engender Health, limetangaza mkakati wa kuimarisha huduma za afya ya uzazi kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu nchini.

Shirika hilo linalotekeleza Mradi wa SuFP limekuja na mkakati huo ili kuyawezesha makundi hayo kupanga uzazi kwa njia salama, kupunguza matukio ya ukatili wa kijinsia na kuongeza uelewa na upimaji wa virusi vya Ukimwi.

Mratibu wake mkoani Tanga, Loveness Malisa, akizungumza jana wakati wa warsha ya kujenga uwezo kwa watoa huduma shirikishi na jumuishi ngazi ya jamii wapatao 23, alisema kupitia mradi huo wanataka utoaji wa huduma zinazozingatia mahitaji ya makundi mbalimbali katika jamii. Engender Health wanatekeleza mradi huo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Seikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Afya (MoH).

"Mradi huu wa SuFP vilevile unatoa huduma jumuishi na shirikishi kwa watu wenye ulemavu," alisema Malisa.

Alisema shirika hilo linafanya kazi katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara ukiwamo wa Tanga kwa kutoa huduma jumuishi, shirikishi, kuimarisha mifumo ya afya na kuwajengea uwezo watoa huduma za afya.

Malisa, alisema warsha hiyo inalenga kukuza uelewa kuhusu haki na ustawi wa watu wenye ulemavu, kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuwajumuisha watu wenye ulemavu katika kila nyanja ya maendeleo, ikiwamo afya, elimu na ajira.

Alitaja malengo mengine kuwa ni kutathmini maendeleo katika utekelezaji wa sera na mikakati ya kuhakikisha usawa na ujumuishaji wa watu.

Malisa, alisema wakati wakiadhimisha siku hiyo, wanakumbushwa ujumuishaji na ushirikishaji wa watu wenye ulemavu kuwa si jukumu la mtu mmoja, bali ni la watu wote.

Akizungumzia mchango wa EngenderHealth kupitia SuFP, alisema kama mradi wamekuwa wakitoa huduma za afya ya uzazi ambazo ni jumuishi na shirikishi ambazo hazibagui mtu yeyote.

Alisema wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha huduma za afya ya uzazi zinapatikana wakati wote kwa kila mtu bila kujali hali yake. Malisa alitaja baadhi ya changamoto kuwa ni idadi ndogo ya watoa huduma waliopata mafunzo ya huduma jumuishi na shirikishi kuhusu watu wenye ulemavu.

Nyingine ni mfumo wa kukusanya taarifa za afya (MTUHA) kushindwa kutambua kikamilifu watu wenye ulemavu wanaopata huduma.

Shirika hilo ili kuimarisha huduma limetoa mapendekezo kwa serikali kuweka mfumo wa mafunzo kwenye mitaala ya vyuo vya afya ya huduma shirikishi ya wanafunzi wa kada ya afya.

Mapendekezo mengine ni kuboresha miundombinu katika vituo vyote vya afya ili viwe na miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu na kutaka mafunzo kazini (OJT) yatolewe mara kwa mara kwa watoa huduma kuhusu huduma shirikishi kwa watu wenye ulemavu na kufundisha matumizi ya lugha za alama kwa watoa huduma wa afya vituoni.

Malisa kwa niaba ya EngenderHealth, alitumia fursa hiyo kuishukuru serikali kwa kujenga vituo vingi vya afya na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa jamii, wakiwamo watu wenye ulemavu.

Ofisa Utetezi kutoka Youth With Disability Community Program, Prisca Mwakasendile, alizitaja baadhi ya aina ya ukatili wa kijinsia kuwa ni wa kingono, uchumi, vipigo na unyanyapaa.

# Mazingira Kilimanjaro yatunzwe, DC Timbuka

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Dk. Christopher Timbuka, amemtaka kila mwananchi kutunza mazingira ya Mlima Kilimanjaro ili kulinda uoto wa asili na barafu.

Timbuka alitoa kauli hiyo juzi wakati akiwaaga wapanda mlima huo 33, ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya miaka 63 ya Uhuru wa Tanganyika ambayo hufanyika nchini Desemba 9, kila mwaka.

Alisema ametoa rai hiyo kutokana na shughuli za kibinadamu kuathiri barafu ya mlima huo na kuwataka wadau kuendelea na utunzaji wa mazingira.

"Nitoe onyo kwa wananchi wote wanaoshiriki vitendo vya uharibifu wa mazingira kwani kufanya hivyo ni chachu ya uharibifu wa barafu ya Mlima Kilimanjaro, watu wote tunajukumu la kutunza mazingira," alisema Timbuka.

Kwa lango la Lomosho ni mara ya pili kwa kampuni ya African Senic Safaris kupandisha watalii.

Takwimu zinaonyesha kuwa mwaka jana kampuni hiyo ilipandisha watalii 11 katika mlima huo na kwa mwaka huu wa 2024 ni 24. Ongezo hilo ni sawa na asilimia 100.

Takwimu hizo zinaonyesha kuwa mwakani idadi ya watu watakaopanda mlima huo itaongezeka mara dufu baada ya kupata mwamko kutokana na historia nzuri ya mlima huo.

Kamishina wa Uhifadhi Kanda ya Kaskazini, Beatrita Lyimo, alisema lengo la kupanda mlima ni kukumbuka mema yaliyofanywa na waasisi wa nchi ya Tanzania ikiwa ni pamoja na kutangaza vivutio vya utalii.

"Utalii unatukutanisha pamoja, tunaongeza umoja na mshikamano, Unakuza pato la nchi na unasaidia maendeleo, hivyo ni wajibu wa kila mmoja kujikita katika kutangaza mazingira," alisema Beatrita.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Utali ya African Senic Safari, Nsimbo Natai, alisema wamekuwa wakitumia lango hilo la Lemosho kufika kileleni Kilimanjaro.

Natai, alisema wapanda mlima huo hutumia lango hilo kufika kileleni kwa siku saba.

Alisema kwa kutumia lango hilo, watalii hupata fursa ya kuzunguka mlima huo, kujionea mandhari ya uzuri wa mlima na kuuliza maswali.

"Njia hii ni ndefu, lakini inamfanya mtu kuzoea mlima na uwezekano wa kufika kileleni ni asilimia 99, na pia watapata nafasi ya kuona kanda mbalimbali za mlima ikiwamo ya janga, msitu na barafu," alisema.

Baadhi ya wapanda mlima huo, akiwamo Bahati Nyakiraria, alisema amejiandaa na kutokana na wingi wa siku anategemea kufika kileleni.





# Wakulima wa tumbaku wajitibulia kimataifa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA wa tumbaku wa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wameshauriwa kutumia mbolea na viuatilifu vya kutosha kupata mavuno na kuhimili ushindani katika soko la kimataifa kwa ubora.

Ofisa Kilimo wa Kampuni ya Mkwawa, Shaban Katete alitoa ushauri huo kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 31 wa Chama cha Msingi Uyogo kilichopo Kata ya Uyogo-Ushetu.

Katete alisema kuwa ametoa ushauri huo baada ya kubaini kuwa licha ya wakulima kupewa ruzuku ya pembejeo, wamekuwa hawazingatii matumizi sahihi kama wanavyoelekezwa na wataalamu wa kilimo na kuharibu ubora wa zao hilo katika soko hilo la kimataifa.

Alisema baadhi ya wakulima hawatumii vema mbolea na viuatilifu katika tumbaku na badala yake wanaweka kiasi na kingine kwenye mahindi na mazao mengine na kukosa tumbaku bora.

Katete, alisema msingi wa uzalishaji wa tumbaku upo kwenye mbolea na viuatilifu.

Alisema tumbaku inapokosa mbolea ya kutosha, mavuno yanakuwa kidogo na inakosa rangi ya kijani ambayo inahitaji.

Aliwataka wakulima kuacha tabia hiyo mara moja na kuzingatia ushauri wanaopewa na wataalamu kila msimu wanapowatembelea mashambani.

Mwenyekiti wa Uyogo, Maganga Masanja, alisema amekuwa akiwahimiza wakulima kutumia mbolea vema kwenye zao hilo kupitia vikao vya kawaida na mkutano mkuu wa mwaka.

Masanja, alisema amekuwa akiwakumbusha kufuata maelekezo ya wataalamu wa kilimo ili kupata mavuno ya kutosha na tumbaku yenye ubora na kukabiliana na ushindani katika soko la kimataifa.

# Nishati ya gesi ya bei chee yaja

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KILIO cha muda mrefu cha wananchi kuhusu gharama ya bei ya mitungi ya gesi ya kupikia kuwa juu na baadhi yao kushindwa kumudu kimesikika.

Ni baada ya serikali kuanza kutoa majiko hayo kwa nusu bei kwa lengo kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia majumbani na kuachana na kuni na mkaa ili kutunza mazingira.

Majiko hayo yanatarajiwa kutolewa na kuuzwa kwa nusu bei na Wakala wa Nishati ya Umeme Vijijini (REA) huku Mkoa wa Mwanza ukitarajiwa kusambaziwa mitungi ya kilo sita 19,530, kila wilaya ikitarajiwa kupata 3,255.

Mpango huo wa serikali umebainishwa na Mhandisi Mwandamizi wa REA, Deusdedith Malulu jijini Mwanza.

Kwa mujibu wa Malulu, serikali itagharamia Sh.bilioni 8.6 ikiwa na azma ya kufikia malengo ya matumizi ya asilimia 80 ya nishati hiyo safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

**Kwa mujibu wa Malulu, serikali itagharamia Sh.bilioni 8.6 ikiwa na azma ya kufikia malengo ya matumizi ya asilimia 80 ya nishati hiyo safi ya kupikia...**

Mitungi hiyo itauzwa kila wilaya 3,255 kwa Sh. 20,000 badala ya Sh.40,000 huku nusu nyingine ya gharama inatolewa na serikali kupitia ruzuku.

Mradi mwingine utakaogharamiwa na serikali ni wa usambazaji wa nishati ya umeme wa jua ambapo itauzwa kwa bei ya ruzuku ya asilimia 75 kwa wananchi waishio visiwani ambao watapata kwa Sh.100,000 hadi Sh. 200,000 badala ya makadirio ya Sh.600,000.

Mradi wa tatu ni wa utoaji wa mikopo yenye masharti na riba nafuu kuwawezesha wananchi kujenga vituo vidogo vya mafuta maeneo ya vijijini ili kurahisisha huduma hiyo katika maeneo hayo.

"Tunatarajia kukopesha kuanzia Sh. milioni 133 kwa masharti nafuu na waombaji wote wanashauriwa kutembelea tovuti yetu ya www.rea.go.tz na watakutana na bango linalojieleza," alisema Malulu.

Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Chagu Nghoma, alisema ruzuku katika nishati hizo ni muhimu na kuwataka wananchi kuchangamkia fursa hiyo.



Baadhi ya wanachama wa Shirika la Haki Sawa kwa Wote lenye maskani yake, mjini Musoma, mkoani Mara, wakiwa katika maandamano ya amani juzi, kuadhimisha Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaume sasa walilia ajenda ya ukatili kijinsia

**Na Alex Sayi,** MASWA

BAADHI ya wanaume mkoani Simiyu wametaka ajenda ya kudhibiti vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi yao ipewe kipaumbele badala ya kuegemea kwa wanawake na watoto pekee na kuendelea kudhalilika katika jamii.

Rai hiyo inakuja wakati Maadhimisho ya Kampeni ya Kimataifa ya Siku 16 Kupinga Ukatili wa Kijinsia Duniani kujikita zaidi kwa wanawake kuanzia Novemba 25 hadi Desemba 10 kila mwaka.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wanaume hao walitaja baadhi ya vitendo hivyo kuwa ni wenzi wao kuwalaza mzungu wa nne kwa madai ya haki sawa kwa wote.

Mkazi wa Kijiji cha Ngeme wilayani Meatu, Sita Mayunga, alisema kuna wanawake hawataki kujamiiana na waume zao kama njia ya kuwakomoa.

Mkazi wa Kijiji cha Mwaukoli wilayani Meatu, Petter Samwel, alisema kuna wanawake wanatumia tafsiri potofu ya haki za binadamu kunyanyasa waume zao.

"Haki za binadamu wanawake wamekuwa wakitumia kama fimbo kuwaadhibu waume zao," alisema Samwel.

Mkazi wa Machinjioni wilayani Maswa, Daniel John, alidai katika kila kaya 10, mbili wanaume wananyimwa unyumba na wake zao.

Simba Jiyunga, Mkazi wa Kijiji cha Nkololo wilayani Itilima, alidai wanaume wengi wanapita katika wakati mgumu, lakini hawajitokezi kutoa ya moyoni hadharani.

Mkazi wa Mtaa wa Majebele Kata ya Nyalikungu, Maswa, Esther Walwa, alidai wanaume kunyimwa unyumba na wake zao kunatokana na kukosa uaminifu katika ndoa kwa kuwa na wake wengi.

Ofisa Mwanasheria wa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Maswa, Fedrick Mussa, aliwataka wanaume kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia wanaotendewa na wake zao.

"Waache kubaki na mambo kifuani na kulalamikia sheria za haki za binadamu ambazo zinazowalinda wote, wanaume na wanawake, ni vema wakaripoti matukio hayo," alisisitiza Mussa.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya hiyo, Basilasi Bruno, alisema taarifa za wanaume kufanyiwa ukatili wa kijinsia na wenzi wao zimeendelea kusikika, inagawa hawajitokezi kuripoti.

Mkaguzi Msaidizi, Philipo Felician, wa Dawati la Jinsia wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Maswa, alisema madawati ya kijinsia yaliyopo vituo vya polisi hayana upendeleo, hivyo wanaume wanatakiwa kujitokeza kutoa taarifa za ukatili na unyanyasaji dhidi yao.

ama
ALHAMISI DESEMBA 5, 2024
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

**WIKI YA UKIMWI DUNIANI...**

## Mwaka unatimu ushuhuda wa tukio, nasaha zake Majaliwa bado zinaishi



Ukurasa 14

## Namna ufugaji nyuki unavyounda ubia na mazingira, wanyamapori

WIKI YA UKIMWI DUNIANI...

# Alichowekeza Samia kikao kikuu UN na anachoendeleza miaka mitatu kazini

**Na Mwandishi Wetu**

JUMAPILI ya wikiendi iliyopita ilikuwa na maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani. Ni vita vya dunia, ambayo kila nchi inapigana.

Maadhimisho hayo ya kila Desemba Mosi ya mwaka, nchini yanaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS).

Tanzania ikiwa katika uongozi wa awamu ya sita imeendelea kudumisha vita hivyo, kukiwapo ufafanuzi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan baada ya kuingia madarakani mwaka 2001, alipokaribishwa kuhudhuria kikao cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.

Akihutubia mara ya kwanza kwa njia ya mtandao wakati huo, dunia ikisumbuliwa maradhi ya Covid 19, Rais Dk. Samia akasema: “Ukimwi siyo tena hukumu ya kifo nchini Tanzania kama ilivyokuwa miaka 38 iliyopita.

“Vifo vitokanavyo na Ukimwi vimepungua kutoka elfu 64 kwa mwaka 2010 hadi elfu 32 mwaka 2020. Maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yamepungua kutoka asilimia 18 mwaka 2010 hadi asilimia saba mwaka 2020.”

Mkutano huo kimataifa ukapitisha azimio la kisiasa lililolenga kuongezwa juhudi za kutokomeza Ukimwi duniani, hoja ambayo Rais Dk. Samia akachangia kwa maoni “Tanzania inaunga mkono mshikamano huo wa kina.”

**ILIVYO SASA**

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Ummy Nderianaga, anayewajibika na kusimamia maadhimisho hayo, anaeleza kuwa Tanzania imepiga hatua katika mapambano dhidi ya Ukimwi.

Hapo anatoa sababu kwamba kasi ya maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU), vimepungua, akirejea wastani wa maambukizi ya awali mwaka 2017 yalikuwa 1,700,000, wakati huo Dk. Samia alikuwa Makamu wa Rais.

Baadaye katika miaka miwili na nusu ya urais wake mwaka jana, 2023, Dk. Samia akiwa rais, takwimu zinashuka hadi 1,540,000.

Naibu Waziri Ummy, ana ufafanuzi wake kwamba maambukizi ya virusi vya Ukimwi nchini inaonekana kuathiri zaidi makundi kama vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 24.

Katika hilo, anayataja makundi maalum ya masafa marefu, wachimbaji wadogo wa madini na wavuvi, wakichangia maambukizi mapya ya ugonjwa huo nchini.

Naibu Waziri Ummy, anataja siri ya mafanikio hayo kupunguza kasi ya maambukizi nchini, ni jitihada chini ya Rais Dk. Samia ikiwamo kuhakikisha huduma bora za tiba na matunzo kwa walioambukizwa virusi vya ugonjwa huo.

Ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa (UNAIDS 2022, inataja Tanzania imefikia Mkakati wa Kimataifa wa UKIMWI 2021 hadi 2026 kwa lengo la matibabu.

Ni hatua nchini inayotajwa kufikia nyanja mbalimbali za mwitikio wa VVU, ambayo yamechangiwa na Matokeo ya Utafiti wa Athari za VVU Tanzania iliyofanyika na UNAIDS, ikitaja kati ya asilimia 82.7 na 97.9 katika ngazi ya jamii.

> “Vifo vitokanavyo na Ukimwi vimepungua kutoka elfu 64 kwa mwaka 2010 hadi elfu 32 mwaka 2020. Maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yamepungua kutoka asilimia 18 mwaka 2010 hadi asilimia saba mwaka 2020.”

Kwa mujibu wa Naibu Waziri Ummy, anasema serikali kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI, mikoa yote nchini imeelekezwa kuandaa na kuadhimisha Siku ya Ukimwi Duniani Desemba Mosi ya mwaka kila mkoa nchi nzima.

"Nichukue fursa kuendelea kuwahimiza wakuu wa mikoa yote kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo katika mikoa yao kusimamia utekelezaji wa shughuli hii na kuhamasisha wananchi katika ngazi zote kwa pamoja tushirikiane kuadhimisha siku hii," anasema.

Kaimu Mkuu wa Programu katika Wizara ya Afya, Dk. Riziki Kisonga, anasema Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, pia wadau walijipanga kutoa huduma mbalimbali katika mazingira ya tarehe 24 mwezi uliopita na kudumu wiki moja hadi kwenye kilele chake, Jumapili iliyopita.

"Huduma ambazo tutazitoa zinahusisha huduma za elimu juu ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na matumizi sahihi ya dawa na kingatiba kwa makundi maalum bila kusahau watoto waliopo katika mazingira hatarishi ya kupata UKIMWI, upimaji wa VVU na magonjwa muambata ikiwamo magonjwa ya ngono na homa ya ini," akatamka Dk. Kisonga.

Kaulimbiu ya Maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani mwaka huu inasema 'Chagua njia sahihi tokomeza Ukimwi'.

•Soma zaidi Uk. 12




Wananchi wa Ifakara, mkoani Morogoro katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, Jumapili iliyopita. **PICHA: MTANDAO**

AFYA

## WIKI YA UKIMWI DUNIANI...

# Mwaka unatimu ushuhuda wa tukio, nasaha zake Majaliwa bado zinaishi

**Na Beatrice Moses**

MWAKA jana Siku ya Ukimwi Duniani, 2023 kitaifa ilifanyika mkoani Morogoro. Hadi sasa ni mwaka mmoja, ambao katika mfano linganishi, kuwapo mtoto mwenye afya njema.

Ni wazi anakuwa amepitia hatua kadhaa za kukua ikiwamo kukaa, kutambaa, kula vyakula kadhaa, kuota meno, kusimama na hata kuanza kupiga hatua za kutembea.

Kihistoria tangu mgonjwa mwenye HIV ajulikane nchini miaka ya mwanzoni mwa 1980 ni takribani zaidi ya miaka 40. Huo tayari ni umri wa mtu mzima ikitarajiwa kuona hatua kadhaa za mafanikio katika maisha yake.

Hivyo, hata katika mapambano dhidi ya maambukizi ya HIV, yanaonyesha kuna mafanikio kiasi. Katika hotuba yake kwenye kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, mkoani Morogoro Desemba Mosi mwaka huo uliopita Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akagusa mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa katika kuendelea kudhibiti maambukizi hayo ya HIV nchini.

"Ili kuumaliza Ukimwi tunapaswa kubadilisha namna tunavyotekeleza afua mbalimbali. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, visababishi vya maambukizi ya Ukimwi, vinahitaji kubainishwa," anafafanua.

"Sio tu kwenye ngazi ya kitaifa, bali kuanzia ngazi ya familia, ambako tabia na mitindo ya maisha zinasababisha maambukizi," anasema Waziri Mkuu katika hotuba yake.

Akaitaka jamii kutumia siku hiyo Desemba Mosi ya kila mwaka itumike kutafakari namna harakati zote za mapambano hayo ya Ukimwi na kaulimbiu za Maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani mwaka wa 2023 'Jamii Iongoze Kutokomeza UKIMWI.'

Anasema, hiyo ni kutokana na msisitizo uliowekwa katika umuhimu wa kutoa nafasi kwa jamii kushika hatamu ya mapambano ya kutokomeza maradhi hayo.

"Changamoto iliyopo katika mapambano dhidi ya Ukimwi ni kwa jamii kutokuwa na ushiriki wa kutosha kwenye kuongoza mwitikio wa Ukimwi," anatamka Majaliwa.

Anabainisha kwamba ni changamoto inayochangiwa na upungufu wa rasilimali kama fedha, utaalamu na kuwapo mazingira magumu ya mwendelezo wa huduma za kinga na tiba dhidi ya VVU.

Ili kufikia Azimio la Kutokomeza Ukimwi Ifikapo mwaka 2030, kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watu (UNAIDS) kuna ufafanuzi ni vema kuendelea kujikita kwenye upimaji VVU, kuwabaini wenye maambukizi na kutoa huduma ya matibabu haraka, pasipo kuchelewa kwa atakayegundulika ana maambukizi hisika ya VVU.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akihutubia kwenye kilele cha Siku ya Ukimwi Duniani, mjini Songea, Ruvuma, mnamo Desemba Mosi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**MWANAHARAKATI**

Nipashe inazungumza na Mwanaharakati Neema Halid, kijana anayeishi na VVU akifanya kazi ya uchechemuzi kwa vijana na wanawake kwenye shirika la DWWT, anayesema kuwa alizaliwa na HIV lakini familia yake ilimficha.

"Nilikuwa nabadilishiwa magonjwa tu, mara leo naambiwa naumwa sukari, mara presha na vitu vingine. Kuna siku tulitoka na marafiki zangu kama wanne kwenda kupima kituo cha Angaza Magomeni (Dar es Salaam). Nilikuwa na umri mdogo tukadanganya miaka," anatamka msimulizi, akiwa pia yumo katika kikundi cha wasichana wanaofanya hamasa na ushauri kuhusu HIV na Ukimwi chini ya usimamizi wa Shirika la Dare.

"Nilikuwa kibonge, tulidanganya miaka. Wenzangu waliletewa vikaratasi vya kurudi, lakini mimi nikaambiwa niende na mzazi wangu. Yule mama aliniambia anajua kuwa nimedanganya umri," anasimulia Neema.

Anaeleza kuwa baada ya kufika nyumbani akamweleza mama yake, lakini mzazi huyo alikasirika na kumkaripia, akimkumbusha alishamwonya asifanye vipimo vyovyote wala kumeza dawa kabla ya kumshirikisha.

Siku iliyofuata walienda kwenye kituo hicho na mama yake, hapo akaujua ukweli kwamba tayari ana maambukizi ya HIV. Mwanaharakati huyo anatolea maelezo akisema:

"Nilimchukia mama sana! Sikutaka kuwa naye karibu, lakini baadaye nilipata nafasi ya kutambua kwamba alishindwa kunishirikisha akijiona kuwa mkosaji.

"Lakini wakati huo hakukuwa na dawa ambazo mjamzito mwenye HIV angekunywa na kumwepusha mtoto na maambukizi."

Anasema akapata hamasa kujiunga kwenye klabu za watoto na vijana kuanzia umri wa miaka 15 hadi 24 na huko alishiriki na kuanza kupata tumaini jipya.

Hiyo ni pamoja na wito wa kujitokeza hadharani kushiriki na kuelimisha jamii kuhusu HIV na Ukimwi na njia bora za kuishi kwa walio na maambukizi, kulingana na uzoefu alionao kwenye hali hiyo.

Kwa mujibu wa Neema, kuna wakati akawa tayari kwenye uhusiano wa kimapenzi na mwenza hata alimweleza ukweli wa hali yake na mpenzi huyo akamkubali.

Hata hivyo, kabla ya hapo alishakutana na vijana waliomtamani na pale alipowaambia ukweli, hawakuwa tayari kuwa naye, wengine walimtenga.

Sasa yupo anahamasisha watu wote kupimwa Ukimwi, wakiwamo wazazi na walezi kuwapima watoto na kuwajulisha tangu umri wa miaka tisa waweze kutambua njia sahihi za kuishi katika hali zao wakiepuka ama kuambukiza au wao kupata mambukizi mapya.

**HALI ILIVYO**

Katika utafiti wa viashiria vya Ukimwi kwa mwaka 2022/2023 uliofanywa na serikali, ikiishirikiana na taasisi kadhaa zikiwamo binafsi, umebaini kuwa watu wanaoishi na VVU (kiwango cha ushamiri) wenye umri zaidi ya miaka 15 ni asilimia 4.4; kaati yao, asilimia 4.1 ni wanapatikana Tanzania Bara na asilimia 0.4. ni wa Visiwani Zanzibar.

Mgawanyo wa kijinsia ulivyo ni kwamba wanawake wako asilimia 5.6, ikilinganishwa na wanaume asilimia 3.0. Pia kwa kuzingatia kigezo cha makazi, maeneo ya mjini ni asilimia tano na vijijini asilimia nne.

Ni utafiti unaobainisha kwamba maambukizi mapya miongoni mwa watu wazima zaidi ya miaka 15 yameendelea kupungua kutoka watu 72,000 waliokuwapo mwaka 2016/2017 hadi watu 60,000 kwa mwaka 2022/2023. Hiyo ni sawa na upungufu wa asilimia 0.18, asilimia 0.24 ni wanawake na asilimia 0.11 wanaume.

Utafiti huo pia umebaini kiwango cha kufubaza VVU kimeendelea kukua na kufika wakati huo wastani asilimia 78. Mgawanyo wake kijinsia, wanawake wako kiwango kimekuwa kwa asilimia 80.9 na wanaume asilimia 72.2; ikilinganishwa na asilimia 52 ya jumla iliyokuwapo katika ripoti ya utafiti mwaka 2016/2017.

Waziri Mkuu Majaliwa anadokeza matokeo ya utafiti huo kwamba, kuna ushahidi wa afua zinazoendelea kufanya vizuri, licha ya kuwapo vikwazo na changamoto zinazoikabili serikali, hata inayoangaza maeneo muhimu yanayohitaji juhudi zaidi," anasema.

Takwimu za hali ya UKIMWI nchini zinaonyesha kundi la vijana na hasa wa kike liko kwenye hatari kubwa ya kupata maambukizi ya VVU, nalo hilo, Waziri Mkuu anaitolea ufafanuzi kwamba:

"Utafiti umebaini kuwa wengi miongoni mwa vijana wanajihusisha kwenye mazingira hatarishi, ikiwamo kufanya ngono zembe, matumizi ya dawa za kulevya na ulevi wa kupindukia."

Pia Majaliwa anaendelea: "Takwimu zilizoko zinaonyesha ukubwa wa tatizo hilo kijamii, hivyo basi, lazima tuwe wabunifu ili kufikia malengo ya kitaifa na kimataifa.

"Watanzania wenzangu, ninapenda sote tufahamu kuwa, kati ya mambo yanayorudisha nyuma juhudi za kudhibiti UKIMWI ni unyanyapaa na ubaguzi."

Anaukemea kwamba ni mtazamo potofu, unaofifisha upatikanaji haki kwa baadhi ya watu kuonekana hawastahili, hata wakatengwa wakichochewa na waoga wa kupima afya zao kwa hiyari kupata usahihi na haki ya kupatiwa huduma za dawa kinga za ARV kwa wanaoishi navyo.

Waziri Mkuu anahitimisha nasaha zake kwa kauli: "Serikali, haitosita kuchukua hatua kwa yeyote atakayebainika kujihusisha na vitendo vya unyanyapaa na ubaguzi," anasema.



Maadhimisho ya kilele cha Siku ya Ukimwi Duniani yakiendana na huduma mbalimbali zinazohusiana.

AFYA

# Dunia ikijadili Sheria Kujiua Uingereza, wadau waitafsiri 'nchini haitekelezeki'

**Na Aidan Mbuguye**

SIKU chache zilizopita umeibuka mjadala uliotoka hisia za watu wengi duniani, baada ya Bunge la Uingereza kupitisha muswada unaoruhusu wagonjwa kusaidiwa kufa.

Kabla ya kupitishwa, kulikuwapo kampeni nchi nzima iliyoanza muda mrefu ikitambulika kwa jina'Campaign for Dignity in Dying', ikimaanisha uhuru wa mgonjwa kuamua kifo na kusaidiwa kufa kifo chema.

Kama muswada huo utapitishwa na bunge kuu la pili, Bunge la Mabwanyenye (House of The Lords), utaifanya Uingereza kuwa mojawapo ya nchi chache duniani zinazoruhusu utaratibu huo.

Nyingine ni Canada, New Zealand, Uhispania na baadhi ya majimbo ya Marekani kama Oregon na California.

Huo ni muswada unaowahusu wagonjwa walio katika hali mahututi na ambao imethibitika kitabibu kuwa hawawezi kupona na muda wao kuishi hauzidi miezi sita.

Imeonekana, muswada huo kuungwa mkono na wananchi wengi waliondamana na mabango na moja ya mabango yalisomeka 'kifo changu maamuzi yangu.'




Wanaharakati wa nchini Uingereza, katika kampeni ya kumruhusu mgonjwa aliyeelemewa, aruhusiwe kuchagua kifo kwa hiari
**PICHA : MTANDAO**

**MAANA YAKE ILIPO**

Je utaratibu wa kusaidia wagonjwa kufa ni nini? Ni utaratibu wa kukatisha uhai wa mgonjwa ili kusitisha maumivu makali anayopitia baada ya kuthibitika kuwa hawezi kupona.

Lengo ni 'kumsaidia mgonjwa kufa kifo kizuri' na mapema, badala ya kumuacha kupitia maumivu makali ya muda mrefu, hatimaye 'anakufa kifo kibaya cha maumivu makali.'

Kunatajwa kuwapo aina mbalimbali za kusaidiwa mgonjwa kufa, ambazo ni: Kusaidiwa kufa kwa hiari; mgonjwa kutoa ridhaa ya kusaidiwa kufa (Voluntary Euthanasia).

Pia kuna: Kusaidiwa kufa bila hiari; mgonjwa anasaidiwa wakati anakuwa kapoteza fahamu na matakwa yake hayajulikani (Involuntary Euthanasia).

Aina nyingine inatajwa na wenye taaluma kuwa ni kumsaidia mgonjwa kufa kwa njia kali, kwa kusitisha uhai wake kwa mfano, kumchoma sindano yenye sumu (Active Euthanasia).

Hapo unasitishwa uhai wa mgonjwa kwa njia batili kwa kuondoa mashine zinazomsaidia mgonjwa kupumua, kuondoa mashine ya chakula au kusitisha matibabu yanayomfanya mgonjwa aendelee kuishi (Passive Euthanasia).

Kuua kumuonea huruma mgonjwa kwa ndugu, kunafafanuliwa na wenye taaluma kuwa ni kufanyika uamuzi ya kusitisha uhai kwa sababu ya maumivu makali anayopitia mgonjwa wao (Mercy Killing) na daktari kumsaidia mgonjwa kusitisha uhai kwa kumpatia dawa ili asitishe uhai wake mwenyewe (physician-assisted suicide).

Pia, katika utaratibu wa kusaidiwa kufa, inatajwa mgonjwa ana haki kuchagua njia itakazotumika kusitisha uhai wake au mtu mwingine, hususani ndugu wa mgonjwa kuchagua na kusimamia njia itakayotumika kusitisha uhai.

**MZIZI WA MJADALA**

Bado kuna mjadala unaoendelea katika jamii, , wengine hawakubaliani na utaratibu wa kusaidiwa kufa, pia wapo wanaokubaliana, lakini wanachopinga ni kumsaidia mgonjwa kufa bila ridhaa yake.

Hapo wanarejea matukio ya mwishoni mwa miaka ya 1930 na mwanzoni mwa miaka 1940, nchini Ujerumani, pale mtawala Adolf Hitler, alipoendesha programu ya kuwaangamiza watoto wenye ulemavu bila ridhaa yao na bila ridhaa ya wazazi wao, kwa kivuli cha kupunguza gharama kwenye jamii.

Makundi tofauti duniani yanayounga mkono suala hilo, yanatoa hoja kwamba "kumsaidia kufa mgonjwa mwenye maumivu na asiyetarajia kupona sio vibaya kama kumuacha afariki kwa maumivu makali ya muda mrefu."

Wengine wanasema kuwa wagonjwa wanapaswa kuwa na haki ya kufanya au kuamua wanachotaka kuhusu maisha yao.

Vilevile, kuna wanaosema wagonjwa ambao wamepoteza fahamu na hawawezi kupona kuwasaidia, kufa kunazuia gharama na jitihada za bure za matibabu.

Ni hoja inayoendelezwa kuwa, kama mgonjwa anateseka, kumsaidia kufa ni kumzuilia mateso. Pia, kuna suala la daktari kumsaidia mgonjwa aliye kwenye hali mahututi ni kumsaidia mgonjwa anayetaka kufa kifo chema.

**UKOSOAJI**

Vilevile, yapo maoni ya pingamizi; wanaokosoa wanasema 'kuua siku zote sio sahihi, haijalishi mgonjwa karidhia au ndugu zake wameridhia lakini yote ni kukiuka haki za mgonjwa na haikubaliki."

Wataaluma wanaohusika na maadili, wana mtazamo kuwa "ni vyema kumuacha mtu afariki na sio sahihi kumuua", kwa kile kinachoitwa "ni kumsaidia kufa."

Kuna wengine wanasema "mwenye haki ya kuondoa uhai wa mtu ni Mungu pekee," huku kuna makundi yenye maswali ya wanaohoji: "Kumsaidia mgonjwa kufa ni vibaya kuliko kumuacha afariki mwenyewe kwa Maumivu, ilihali njia zote zitaleta matokeo yanayofanana?"

**MAONI NCHINI**

Baada ya mitazamo hiyo duniani; kwa wakazi nchini ( majina yao ya pili tunayo) anaionanje hilo? Mama Ester wa Chanika, Dar es Salaam, anaeleza uzoefu wa kuuguza kaka mgonjwa wa maradhi.

Ana simulizi namna ilivyofika hatua amechoka, huku kila kukicha hakukuwapo tumaini la kupona na alikuwa mwenye maumivu makali sana, akioanaisha hali hiyo na kitendawili cha muswada wa sheria hiyo mpya ya Uingereza.

Pia, yupo Nelson...., kutoka Biharamulo, Kagera, anayo simulizio kama ya mtangulizi wake, yeye akiimuuguza mke wake muda mrefu kabla ya mauti.

Anasema, ilifika hatua alikata tamaa na madaktari kwa siri 'walimng'ata sikio' kuwa 'mgonjwa hatoweza kupona ni vyema akamrudisha nyumbani ili kupunguza gharama za matibabu.'

Yeye anapingana na suala la kumsaidia mgonjwa kufa, akisema ni vyema kumuacha afariki mwenyewe.

Rehema anayeishi jijini Mwanza, anasema mgonjwa wake wa karibu alitamani kusaidiwa kufa, figo zilipofeli na alikuwa akisafishwa damu kila wiki na gharama kubwa zilitumika.

Anaendelea kusema ilizua ugomvi, kwani mume wake alitaka asisafishwe akafariki kwa kile alichokisema "pesa zitaisha na hatopona na siku akifariki, familia itabaki na nini?".

Binafsi Rehema, anahimzia kuwapo sheria ya kusaidia watu kufa, akinena "sio mbaya kwa wagonjwa watakaotaka kusaidiwa kufa.

**WADAU WANAOWAJIBIKA**

Dk. Moses Patrick anayepatikana mkoani Kilimanajaro, anasema "kuna wakati tunakuwa wawazi kuwa mgonjwa hatoweza kupona! Hatusemi kama atakufa, ila tunawaambia ndugu kuwa kupona itakuwa ngumu!"

Anasema, kuwapo utaratibu wa kumsaidia mgonjwa kufa kwa mazingira ya nchi bado ni ngumu kukubalika.

Viongozi wa dini pia wametoa neno; kiongozi katika kanisa la Kikristo nchini, anasema kuwa haliruhusu mtu kusaidiwa kufa kwa kile alichosema ni kinyume na maandiko matakatifu.

Pia, ni mamlaka ya kuondoa uhai wa mwanadamu ni 'Mungu pekee.'

Aidha, Shekhe Habibu Seif Hashim wa Tegeta, Dar es salaam; anasema kiimani kwake utaratibu huo akaorodhesha sababu kuu tatu.

Katika ujumla wake, utaratibu unaonekana mgumu kukubalika, kwani ni nchi tatu tu duniani na majimbo mawili ya Marekani yanayoruhusu utaratibu huu hadi sasa.

Barani Afrika, Asia, Amerika ya Kusini, na Australia, nchi zote zinatoka Bara la Ulaya, lenye nchi 50. Hiyo inaonyesha kuwa utaratibu huu umekuwa mgumu kukubalika duniani.

*** Ni uchambuzi binafsi wa mwandishi, wakili wa sheria, akikusanya maoni shirikishi nchini. Anapatikana kwa simu: +255 759447946 na baruapepe: joranherman95@gmail.com**

MAZINGIRA

# Namna ufugaji nyuki unavyounda ubia na mazingira, wanyamapori

## • Malengo uchumi yanavyotoa majibu mazingira

**Na Francis Ndemela, MIKUMI**

UFUGAJI nyuki nchini kwa sasa, unachukua nafasi muhimu, kuimarisha maisha endelevu kimazingira na kuwezesha maisha ya pamoja, kati ya wanyamapori na binadamu.

Ingawa, kiasili umekuwa ukitambulika zaidi kwa faida za kiuchumi husussan za uzalishaji asali, sababu za kiikolojia nazo sasa zinachukua nafasi.

Umuhimu wake kiitaalam unatafsiriwa kwenda mbali zaidi ya kuboresha kilimo, ikitajwa nafasi ya suluhisho kwa changamoto za migogoro ya makazi na kijamii, kati ya binadamu na wanyamapori, mfano tembo na binadamu. Vilevile, kuna nafasi ya mwisho wa safari kuhifadhi bayoanuwai.

Kimsingi, ufugaji nyuki una umuhimu mkubwa kwa afya ya binadamu, kupitia bidhaa zake kama asali na nta.

Ikiendewa mbali, asali hutoa nishati na ina viambata vinavyoimarisha kinga ya mwili, huku ikitumika kwa tiba asili kwenye magonjwa kama mafua na vidonda.

Kwa mfano, asali imeonyesha kuwa na uwezo wa kuimarisha kinga ya mwili. kutokana na sifa zake, kama ilivyochapishwa kwenye jarida la Journal of Functional Foods, toleo la mwaka 2017.

Aidha, asali hiyo ina sifa ya kuwa na virutubisho muhimu kama protini, vitamini na madini kadhaa.



Nyuki wakitengeneza asali. **PICHA ZOTE: FRANCIS NDEMELA.**

### NGUVU YA UCHAVUSHAJI

Nyuki ni miongoni mwa wachavushaji muhimu zaidi katika mifumo ya ikolojia duniani. Wanachangia kwa kiasi kikubwa uchavushaji mimea ya mwituni na mazao.

Inatajwa kuwa zaidi ya asilimia 80 ya mimea ya maua duniani, inategemea nguvu ya uchavushaji.

Pia, nyuki hao bado wanachukua nafasi kitakwimu wakichangia kuchavusha takribani asilimia 70 ya mazao yanayoliwa na watu.

### NAFASI YA WAFUGAJI

Kwa kuunga mkono ufugaji nyuki, watu huchochea uchavushaji unaoimarisha ukuaji mimea yenye afya kwa binadamu, vilevile una tija kwa uzalishaji unaohitajika kwa ajili ya kutunza makazi ya wanyamapori.

Ni kawaida kwa yuki wanapochavusha mimea, wanasaidia kuzalisha tena mifumo ya kiikolojia, ikiwamo misitu, na nyasi.

Bayoanuwai hiyo ina mtazamo wa kuunga mkono aina mbalimbali za wanyama, kuhakikisha makazi yanabaki imara na salama, pia chanzo cha chakula kwa wanyama.

Kwa jamii zinazoishi karibu na hifadhi au mbuga za wanyama, hilo likitajwa kusaidia kuleta uwiano kati ya uzalishaji kilimo na kuhifadhi mifumo asilia.

Ni hatua inayoongozana na kupuguza migogoro kati ya binadamu na wanyamapori.

### MIFANO ILIVYO

Suluhisho bunifu kama 'uzio wa nyuki' safu za mizinga ya nyuki inayozunguka shamba zimetekelezwa katika sehemu mbalimbali Afrika, ikiwamo Kenya na Tanzania.

Ni mizinga inayotajwa kuzuia wanyamapori kuingia shambani, pia inatoa chanzo cha ziada cha mapato kupitia uzalishaji asali.

Faida hizo mbili zinatajwa kuufanya ufugaji huo wa nyuki kuwa njia bora inayopunguza gharama na hatari zinazohusisha migogoro kati ya binadamu na wanyamapori, huku ikikuza maisha yao pamoja kwa amani.

### USHUHUDA WA WAKULIMA

Mkulima kutoka kijiji cha Maharaka wilayani Mvomero, mkoa Morogoro jirani na Hifadhi ya Taifa Mikumi, anasema:

"Mwaka 2013 tulikuwa na programu ya kuzungushia mizinga ya nyuki kwenye mashamba yetu, ili kuzuia wanyama waharibifu.

"Tuliona tofauti kubwa, kwani tembo waliokuwa wanavamia, wakawa wanaogopa sana! Kumbe nyuki walikuwa wanafumuka kutoka kwenye mizinga na kuwang'ata tembo wakawa wanaogopa," anaeleza mkulimaVitus Pango

Anaongeza:"Pia, zile kelele za nyuki kama wanavuma hivi nazo ni tishio kwao."

### NYUKI VS MAZINGIRA

Katika suala la kusaidia matumizi endelevu ya ardhi, ufugaji nyuki bado unabaki kuwa na matumizi kidogo ya ardhi, ikilinganishwa na shughuli nyingine za kilimo, hata kufikia hatua kuwa mbadala wa maendeleo endelevu kwa jamii za vijijini.

Tofauti na kilimo chenye matumizi makubwa ya ardhi ufugaji nyuki hauhitaji ukataji ama misitu au uharibifu wa mazingira asilia, bali unahimiza utunzaji wa mimea inayopandwa na ile asilia, ambayo ni muhimu kwa uchavushaji na uhifadhi wa makazi ya nyuki.

Kwa jamii zilizo katika maeneo yenye wanyamapori wengi, suala la ufugaji nyuki unatajwa kuwa chanzo chao cha mipango ya usimamizi endelevu wa ardhi.

Hapo wakulima wanawezeshwa kupata kipato pasipo bila kuingilia makazi ya wanyamapori au kujihusisha na yanayogusa uharibifu ardhi na mimea, kama vile uwindaji, pia ukataji misitu haramu.

Zao lake huwa ni kuchochea uwajibikaji katika kutunza mazingira, kwani wafugaji nyuki wanategemea afya ya mifumo ya ikolojia, ndipo wanapofanikisha riziki zao.

Lingine ni kuimarisha Uchumi na Kupunguza Umasikini, ufugaji nyuki pia unatoa fursa za kiuchumi, hususani kwa jamii zilizoko pembezoni mwa misitu, ikijumuisha wanawake na wakulima wadogo.

Asali na bidhaa nyingine za nyuki ni kama nta, sumu ya nyuki na maziwa yake, huhitajika kimataifa zikiwapa wafugaji wake chanzo cha kipato cha uhakika.

> "Ndani ya miezi mitatu, pesa iliyopatikana ilitusaidia kununua mahitaji yetu muhimu hapa kwenye eneo letu, ambalo linapakana na mbuga (Hifadhi) ya Mikumi (Morogoro) na mara nyingi wanyama huwa wanaingia kwenye eneo hili" anatamka mdau wake anayejitambulisha kwa jina la Daudi.

Hapo ndipo inaposhauriwa kwamba, suala la kuwawezesha kiuchumi wanajamii, pia ufugaji nyuki kunapunguza shinikizo utumiaji wanyamapori au kujihusisha na shughuli zisizo endelevu, kama uvunaji kuvuka wa rasilimali misitu.

"Kupitia asali tuliyoivuna kwenye eneo letu hili ambalo tuliweka mizinga takribani kumi ya majaribio,tulifanikiwa kuvuna lita 60 za asali.

"Ndani ya miezi mitatu, pesa iliyopatikana ilitusaidia kununua mahitaji yetu muhimu hapa kwenye eneo letu, ambalo linapakana na mbuga (Hifadhi) ya Mikumi (Morogoro) na mara nyingi wanyama huwa wanaingia kwenye eneo hili" anatamka mdau wake anayejitambulisha kwa jina la Daudi.

Akifafanua yu mdau mkubwa wa uhifadhi kijijini Mkata, Kata ya Msongozi mkoani Morogoro, anasema ni hali inayopunguza kwa pamoja uhifadhi, hata athari za mabadiliko ya tabianchi.

Katika ujumla wake, tafsiri kuu ni kwamba maeneo yenye mimea na misitu ni muhimu katika kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, kwa usalama wa ardhi kupitia kunyonya vimelea muhimu, pia inadumisha mzunguko sahihi wa maji ardhini.

### INAVYOKUWA ENDELEVU

Wajibu mojawapo unatajwa katika ufugaji nyuki, wanaosimamia kufuatilia ustawi wa mazingira yake, wakielimisha jamii ustawi wa afya ya mazingira yake.

Katika namna pekee, wafugaji nyuki wanapopata uelewa wa kina wa uhusiano kati ya nyuki, mimea, na mazingira, wanakuwa mabalozi bora wa uhifadhi.

Ni miradi inayotajwa kuweza kukuza mtazamo wa uhifadhi, hata kuwahamasisha wanajamii kulinda wanyamapori na rasilimali zao za asili.

Programu za elimu zinazohusiana na ufugaji nyuki zinaweza pia kuhusisha shule na vikundi vya vijana na kuunda uelewa kuhusu jukumu la wachavushaji na umuhimu wa matumizi endelevu ya ardhi.

Ufugaji nyuki daima hauishii kuingiza kipato, ni chombo chenye nguvu ya kukuza uhifadhi wa mazingira na kuimarisha maisha ya pamoja, kati ya binadamu na wanyamapori, ikisaidia matumizi endelevu ya ardhi

**•Mwandishi, pia ni Mshauri Elekezi katika taasisi inayohusika na mazingira, mabadiliko ya tabianchi na uhifadhi wa wanyamapori. Kwa maoni anapatikana kwa baruapepe: francisndemela@gmail.com**



**HABARI DODOMA**

# Serikali, CCM yawafariji waathirika wa mvua Ikungi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI kwa kushirikiana na Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida imetoa msaada wa mahitaji ikiwemo mabati, magodoro na vyakula kwa kaya 24 za waathirika wa mvua wilayani Ikungi.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego na Mwenyekiti wa CCM Mkoa Singida, Martha Mlata, ambao waliambatana na viongozi wengine wa chama na serikali walikabidhi misaada hiyo kwa wananchi wa kata za Mungaa na Makiungu wilayani Ikungi ambazo zimeathiriwa na mvua.

Vitu vilivyokabidhiwa ni mabati 240, magodo 30, magunia 20 ya mahindi, sabuni katoni nne, sukari, unga, maharage na fedha Sh.200 000

Mkuu wa Mkoa Singida, Dendego akizungumza kabla ya kukabidhi vitu hivyo aliwapa pole waathirika hao na kusema serikali ipo pamoja nao na itaendelea kufanya tathimini zaidi kujua mahitaji yao.

**Muswada huo unalenga kuboresha mazingira ya uwekezaji Tanzania na kuimarisha mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya uratibu na usimamizi wa uwekezaji nchini pamoja na kuimarisha masharti....**

Aliwaomba wadau walioguswa na tatizo hilo kuwaunga mkono waathirika kwa kuwapatia mahitaji ili kuwafariji na kuwawezesha kurejea katika hali zao ikiwemo kurekebisha nyumba zao.

Aidha, aliwahimiza vijana wilayani humo kuwasaidia wazee ambao hawana uwezo wa kurekebisha baadhi ya nyumba zao ambazo zina uwezekano wa kurekebishika.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Mkoa wa Singida, Yohana Msita, akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa Singida, Martha Mlata, aliwapa pole waathirika hao na kusema chama kitaendelea kuwasaidia.

Akizungumza kwa niaba ya waathirika wenzake, Beatrice Malaki alisema mvua ya mawe iliyoambatana na upepo iliyonyesha Novemba 30, 2024 imeleta madhara makubwa ikiwemo kubomoa nyumba na kuezua paa katika kijiji cha Kiku.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, akizungumza alipofanya ziara ya kikazi katika Ofisi za Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), iliyolenga kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la ofisi hiyo, jijini Dodoma, juzi. **PICHA: UTUMISHI**

# AG ahimiza weledi, ubora katika kazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Hamza Johari amewataka watumishi wa ofisi yake kusimamia misingi ya weledi na ubora katika utekelezaji wa majukumu yao, ili kuongeza imani kwa wananchi.

Alitoa wito huo juzi jijini hapa, wakati wa kikao maalumu na watumishi wa ofisi hiyo kilichofanyika ukumbi wa Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao hicho, Johari alisema lengo la kikao hicho ni kufahamiana na kuwakumbusha watumishi kanuni na taratibu zinazopaswa kuzingatiwa katika utekelezaji wa majukumu yao, ili kuwa taasisi inayoaminika na umma.

"Ilikuwa ni muhimu sana kuwa na kikao kama hiki ili tuweze kufahamiana vizuri na kuweza kuendelea kufanya kazi vizuri na kila mtumishi ajisikie vizuri kufanya kazi kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

"Nitaendeleza yote mazuri na kuleta mabadiliko chanya ambayo yataweza kutusaidia kama taasisi kutimiza malengo yetu na malengo ya taifa, pia kuifanya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali a place to be", alisema Johari.

Aidha, alisema kupitia kikao hicho ni matarajio yake kuwa watumishi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wataboresha utendaji kazi wao kwa kutoa huduma iliyo bora kwa wakati na kuzingatia maslahi ya taifa.

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Samwel Maneno aliwasisitiza watumishi wa ofisi hiyo kufanya kazi kwa kuzingatia na kufuata dhima, dira, kaulimbiu na maadili ili kuleta matokeo chanya katika utendaji kazi.

Alisema: "Niwaombe watumishi wote wa ofisi hii, tuendelee kuzingatia na kufuata dira, dhima na maadili ya msingi ili tuifikie kauli mbiu yetu ya weledi na ubora".

# Wataalamu mipangomiji wakutana kupanga mipango

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SIKU moja baada ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi kubaini wimbi la maeneo ya huduma za kijamii kubadilishwa matumizi, wataalamu wa mipango miji wamekutana jijini Dodoma kuweka mikakati namna ya kuhakikisha mipango iliyowekwa inadumu.

Akizungumza jana kwenye mkutano mkuu wa tisa wa mwaka wa maofisa mipangomiji Tanzania, Msajili wa Bodi ya Usajili wa Wataalamu wa Mipangomiji, Lucas Mwaisaka, alisema katika mkutano huo wataalamu hao wanajifanyia tathmini na kupata elimu ya namna ya kusimamia mipango wanayoipanga ili kuondokana na tatizo hilo.

"Tumejadili namna ya kutumia teknolojia kusimamia shughuli zote za mipango miji, tumefanya kazi kubwa ya kuanzisha mfumo ambao umeunganishwa na e-ardhi ili kudhibiti na kufanya kazi kwa haraka kuwahudumia wananchi kupitia mifumo,"alisema.

Alisema tangu bodi hiyo ianze kufanya kazi mwaka 2009 imesajili kampuni 101 na wataalamu 546, huku kampuni 11 na wataalamu 32 wamefutiwa usajili kutokana na kukiuka sheria ya mipango miji kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi (NLUPC), Joseph Mafuru, alisema upimaji na upangaji shirikishi wa moja kwa moja kwa wananchi kwenye mitaa na vijiji nchini ndiyo mwarobaini wa kuondokana na wimbi la ubadilishaji wa matumizi ya ardhi iliyopangwa.

Alisema kuna umuhimu kusimamia mipango miji kuanzia kwa wananchi kwenye mitaa husika ili kuimarisha na kulinda maeneo hayo yasibadilishwe matumizi.

"Tumejifungia hapa wataalamu kuangalia njia gani tutumie kwenye 'development control' hili ni muhimu kwa sasa kama mtakumbuka kuna wakati Jiji la Dar es salaam waliweka utaratibu wa kubandika kwenye mitaa ramani ya mipango miji ambayo ilikuwa inaonesha maeneo ya makazi, biashara, viwanja vya michezo, maeneo ya kupumzikia, shule, hospitali na huduma zingine za msingi, hii inasaidia kuwafanya wananchi wa eneo husika kulinda maeneo hayo muhimu kwenye mitaa yao," alisema.

Katibu wa Chama cha Wataalam wa Mipangomiji (TITA), Emanuel Luhamba, aliomba serikali kutoa kipaumbele kwenye sekta ya ardhi hususani kwenye mipangomiji kwa kuwa ni uumbaji mwingine wa pili baada ya Mungu.

Alisema: "Kuna changamoto kubwa zinaikumba sekta ya mipangomiji ikiwamo uhaba wa rasilimali fedha ambazo zingewezesha kupima na kupanga miji yetu na vijiji kwa kuwa vijiji vya leo ndio miji ya kesho, fedha hizi wakati mwingine zinahitajika katika kutwaa maeneo ili yawe wazi uweke mipangomiji inayofaa".





# KKKT yazindua mradi kuwasaidia wenye ulemavu

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

KANISA la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) limezindua mradi wa "Pamoja Tuyajenge" ukiwa na lengo la kutoa elimu kwa watu wenye ulemavu na ukatili wa kijinsia kwa kuwa makundi hayo yanakabiliwa na matatizo ya unyanyapaa kwenye jamii.

Uzinduzi huo ulifanyika juzi katika Halmashauri ya Mji wa Makambako ambapo mradi huo uliopo chini ya idara ya vijana wa KKKT taifa.

Wakizungumza baada ya uzinduzi huo, baadhi ya watu wenye ulemavu mjini Makambako, Rose Masegense alisema licha ya jitahada zinazofanyika ili kukabiliana na vitendo vya ukatili bado kuna tatizo la kutosikilizwa na baadhi ya taasisi binafsi na zile za serikali hasa pale wanapohitaji huduma.

"Ukienda kwenye ofisi za serikali kusikilizwa inakuwa shida na kwenye taasisi hizi binafsi utakapoingia wakajua ni mlemavu wa aina fulani au umeshikiliwa wanakuwa na ile dhana umekwenda kuomba, hivyo tunaomba waondokane na hiyo dhana mbaya," alisema Rose.

**"Ukienda kwenye ofisi za serikali kusikilizwa inakuwa shida na kwenye taasisi hizi binafsi utakapoingia wakajua ni mlemavu wa aina fulani au umeshikiliwa wanakuwa na ile dhana umekwenda..."**

Magadalena Kinyunyu alisema bado kuna baadhi yao wanafungiwa ndani hali inayosababisha wakose haki zao, huku wakiomba kuwezeshwa mitaji itakayowasaidia kuanzisha miradi ya kiuchumi na kuachana na tabia ya kuwa ombaomba.

Naye Ofisa Ustawi Jamii Halmashauri ya Mji wa Makambako, Maria Mkude, alisema bado kuna vitendo vya ukatili kwa watu wenye ulemavu, huku wakitaka jamii kuacha tabia ya kuwafungia ndani watoto wenye ulemavu na kuripoti kwenye mamlaka husika wanapokutana na matukio hayo.

Baadhi ya viongozi wa kidini, Shekhe Ibrahaim Chang'a, alisema jamii inapaswa kushirikiana ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanaishi katika mazingira rafiki ambayo yanawawezesha kupata mahitaji yote ya msingi bila kutengwa.

Naye Mchungaji wa Kanisa la Moraviani, Ezekia Mwashibanda aliitaka jamii kutowabagua watu wenye ulemavu ili kuweza kupata haki zao.

Awali wakitambulisha mradi huo, Mwenyekiti wa Vijana wa KKKT Taifa, Anania Ndondole, alisema wamekuja na kampeni hiyo ambayo itatekelezwa kwa mwaka mmoja kutokana na watu wenye ulemavu kufanyiwa ukatili wa kunyanyapaliwa hata kuzuiliwa kuhudhuria kwenye nyumba za ibada.

"Watu wenye ulemavu ni moja ya kundi ambalo halijapewa kipaumbele cha kutosha katika masuala mengi, iwe katika masuala ya uongozi, iwe katika masuala mbalimbali ya kijamii lakini ndilo kundi ambalo limeathirika na vitendo vya ukatili wa kijinsia," alisema Ndondole.

Ofisa Tarafa ya Makambako Wilaya ya Njombe, Frola Nyato, aliwataka wadau kushirikiana na serikali hasa kuwaibua watu wenye ulemavu ambao bado hawajafikiwa na kuhakikisha wanapelekwa shule.



Mkurugenzi wa Miradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), John Steven (kulia), akizungumza na mmoja wa wanufaika wa mfuko huo, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Watu wenye Ulemavu Duniani, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: FAUSTINE FELICIAN**

# Mradi wa maji kuleta neema wananchi 100,000

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

WANANCHI zaidi ya 100,000 wanatarajia kunufaika na mradi wa maji wa miji 28 katika kata tatu za Halmashauri ya Mji wa Njombe ambazo ni Mji Mwema, Njombe Mjini na Ramadhani.

Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Halmashauri ya Mji wa Njombe (NJUWASA), Robert Lupoja aliyasema hayo juzi katika eneo la mradi la ujenzi wa matangi katika Mtaa wa Lunyanywi.

Lupoja alisema kuwa mradi huo unajengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 40 na unatarajia kuwaondolea adha wananchi kuhusu upatikanaji wa majisafi na salama.

Alisema kata hizo zinawakazi wapatao 91, 000 na mahitaji yao ya maji kwa siku ni lita milioni 10 lakini Njuwasa inazalisha lita milioni tano kwa siku, hivyo kuna upungufu wa maji lita milioni tano hali inayosababisha kuwapo kwa mgawo wa maji wa siku mbili hadi tatu kwa baadhi ya maeneo.

Alifafanua kuwa mradi huo ukikamilika utaongeza kiwango cha maji hadi lita milioni 17 kwa siku hali itakayosaidia kuongeza uwezo kwa Njuwasa kutoa huduma kwa muda wa saa 24 kwa siku zote kwa juma.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa alisema mradi huo utahudumia Halmashauri ya Mji wa Makambako na Njombe ambapo ameridhishwa na hali ya utekelezaji wa mradi huo na kumtaka mkandarasi kuongeza kasi ya utekelezaji kwa kufanya kazi kwa sehemu zote Tatu.

Alisema: "Nakuomba mkandarasi utoe fursa za kupata zabuni za bidhaa za ujenzi ili wazawa waweze kunufaika na fedha za mradi huu na kuongeza mzunguko wa fedha Mjini Njombe na kuona manufaa ya uwepo mradi huu katika wilaya yetu".

# Wanufaika wenye ulemavu TASAF waishukuru serikali

**Na Faustine Feliciane**

WANUFAIKA wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ambao ni watu wenye ulemavu wameiomba serikali kuendelea kulisaidia kundi hilo, huku wakisema mfuko huo umekuwa msaada na kubadilisha maisha yao.

Hivyo, wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuuongezea uwezo mfuko huo ili kuwafikia watu wengi zaidi.

Akizungumza wilayani Kibaha mkoani Pwani, mmoja wa wanufaika ka hao ambaye ni mlemavu, Amina Mrupe, alisema awali walikuwa wakipitia changamoto kubwa kutokana na hali zao, lakini uwepo wa ruzuku hiyo ya TASAF imewabadilishia maisha yao.

"Tunamwomba Rais Samia kuiongezea nguvu TASAF ili kuwafikia watu wengi zaidi, tuna uhitaji mkubwa kutokana na hali zetu hivyo tunaendelea kuiomba serikali kuendelea kutusaidia," alisema Amina.

Alisema kupitia TASAF wameweza kuanzisha biashara mbalimbali kama vile kuuza karanga, kutengeneza batiki, viungo vya chai, chakula pamoja na sabuni na kupitia biashara hizo wamekuwa wakipata fedha kujikimu kimaisha.

Alisema mbali ya kupewa ruzuku hiyo ya kila mwezi ambayo walikuwa wanapatiwa kila baada ya miezi miwili pia amepewa mtaji wa Sh.500,000 ambazo zimemwezesha kuanzisha biashara ya batiki pamoja na kuuza karanga.

"Maisha yamebadilika siyo kama zamani, sasa hivi napata mahitaji yangu muhimu mimi na familia yangu, ndiyo maana tunaiomba serikali kutuangalia kwa karibu watu wenye ulemavu lakini pia kuiongezea nguvu TASAF, kwa kweli inatusaidia sana," alisema.

Mnufaika mwingine, Nuru Ally mkazi wa Kigogo jijini Dar es Salaam ambaye ni mlemavu kutoona alisema kwa sasa ameondolewa kwenye orodha ya wanufaika wa mfuko huo baada ya hali yake ya kiuchumi kuimarika.

Alisema kupitia TASAF ameweza kuwa na ujuzi wa anatengeneza viungo vya chai, viungo vya chakula na sabuni ya chooni na hivyo kuendesha maisha yake. Alisema walemavu wamekuwa wakionekana kama wanapenda kuwa ombaomba lakini kupitia TASAF amekuwa akifanya shughuli zinazomuingizia kipato na kuweza kuhudumia familia yake akiwa na watoto wanne.

Hata hivyo wanufaika hao walisema changamoto kubwa waliyonayo ni soko la kuuza bidhaa wanazozizalisha.

# Wanafunzi watoro 35,000 warejeshwa shuleni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZAIDI ya wanafunzi 35,000 wamerejeshwa shuleni visiwani hapa baada ya kuboresha mazingira ya kusomea na kujifunza.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Hassan Ali Gulamu, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alikuwa akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah Ameir aliyetaka kujua tathmini ya utoro wa wanafunzi shuleni visiwani hapa mpaka sasa.

Gulamu, alisema changamoto ya utoro wa wanafunzi shuleni imepungua kwa kiasi kikubwa ikilinganisha na miaka miwili iliyopita baada ya kuchukua hatua za kukabiliana nazo.

Alisema serikali imefanikisha kufanya hivyo kuwarejesha wanafunzi waliotoroka kupitia mpango wa kuwarejesha watoto shule.

Alisema mafanikio hayo yamekuja baada ya juhudi za serikali kuimarisha miundombinu kwa kujenga shule za ghorofa huku miundombinu ikiendelea kuimarika siku hadi siku.

"Shule hizi pamoja na kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani, zimesaidia kuongeza ufanisi wa kufundisha na kujifunza kwa kuwa na huduma za kisasa zikiwamo maabara za sayansi, kompyuta na maktaba," alisema.

Naibu waziri huyo, alisema ujenzi wa shule hizo unasaidia kupunguza idadi ya wanafunzi katika madarasa na kupata mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia.

# 'Harusi zinashusha hadhi noti ya Tanzania'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Fedha na Mipango imesema noti ya Tanzania inachakaa kwa matumizi mabaya kutokana na wimbi la sherehe za harusi nchini.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Juma Makungu alisema kuwa baadhi ya watu wamekuwa na tabia ya kurusha kwa wahusika noti baada ya kuanguka sakafuni, kukanyagwa, kuziviringisha katika maumbo, kutumika kama mapambo na kuweka kwenye mwili wa mtu wenye jasho na kusababisha kuchakaa na kukosa hadhi

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah Amer, aliyetaka kujua matumizi haramu ya noti hizo na hatua zinazochukuliwa kwa mtu anayeidhalilisha na kushusha thamani noti hiyo.

**"Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda kuufahamisha umma kwamba kuharibu noti au sarafu, au kuonesha dharau au dhihaka kwa noti au sarafu za Jamhuri ya Muungano ni kosa la jinai**

Makungu, alisema vitendo hivyo vinapoteza sifa ya noti ya Tanzania ambayo ni moja ya tunu za taifa.


Alisema vtendo hivyo vinaendelea kutokea licha ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na viongozi wa Serikali kwa nyakati tofauti kukemea.

"Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda kuufahamisha umma kwamba kuharibu noti au sarafu, au kuonesha dharau au dhihaka kwa noti au sarafu za Jamhuri ya Muungano ni kosa la jinai kwa mujibu wa kifungu namba 332A cha kanuni ya adhabu sura ya 16 kama ilivyorejewa mwaka 2002," alisema.

Makungu, alisema mwananchi atakayetenda kosa hilo kwa makusudi anaweza kushtakiwa kwa kosa la jinai na kupewa adhabu ya kulipa faini au kuhukumiwa kutumikia kifungo jela.

Alisema kama kosa limefanywa na mtumishi wa umma, anaweza kupewa adhabu ya nidhamu ikiwamo kufukuzwa kazi au kuondolewa katika nafasi yake.

Hata hivyo, Makungu, alisema serikali inatoa rai kwa wananchi kuhifadhi fedha kwa kuwa ni tunu na alama muhimu ya uchumi wa nchi, kuondoa uwezekano wa kuchakaa mapema na kuipunguza gharama za uchapishaji.



Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Zanzibar, Dk. Khalid Salum Muhammed (kushoto), akizungumza na Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), Stephen Wasira baada ya kutembelea katika Baraza la Wawakilishi, Chukwani juzi. **PICHA: MPICHAPICHA WETU**

# Wenye ulemavu wataka mazingira rafiki uchaguzi mkuu mwakani

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imetakiwa kuwawekea mazingira rafiki watu wenye ulemavu nchini ili waweze kushiriki kikamilifu katika uchaguzi mkuu mwakani.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar, Salma Saadat Othman, katika Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Watu wenye Ulemavu Duniani yaliyofanyika Viwanja vya Gombani ya Kale, Wilaya ya Chakechake Mkoa wa Kusini Pemba.

Salma, alisema wao ni sehemu muhimu ya jamii na kwamba wanaridhishwa na hatua za kuwasaidia zinazochukuliwa na serikali hizo za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuboresha maisha yao kama ilivyo kwa watu wengine.

Alisema pamoja na mambo mengine, mahitaji yao kwa sasa ni kuandaliwa miundombinu rafiki na kuwekewa mazingira bora ya kushiriki katika uchaguzi huo wa rais, madiwani, wabunge na wawakilishi katika majimbo mbalimbali nchini.

Awali akizungumza katika maadhimisho hayo, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, aliitaka jamii kuzingatia haki kwa watu wenye ulemavu ili kuwajengea mazingira bora ya maisha na kutoa fursa sawa kwa wote kukuza, kuimarisha, kuleta maendeleo na kujenga uchumi wa nchi.

Othman, alisema serikali imewaongezea watu hao wenye ulemavu nguvu katika vyombo vya maamuzi kwa ajili ya maendeleo ya nchi kulingana na kaulimbiu ya maadhimisho hayo kwa mwaka huu.

Aliitaja kauli mbiu hiyo kuwa ni 'Kukuza uongozi wa Watu wenye ulemavu kwa mustakabali jumuishi na endelevu'.

Alisema kauli mbiu hiyo vilevile, inahimiza haki na fursa sawa kwa kundi hilo la jamii.

Alitaja mambo hatarishi kwa sasa na kuchangia kiasi kikubwa ongezeko la watu wenye ulemavu kuwa ni magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza yakiwamo kisukari na wimbi la ajali za barabarani.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, katika salamu zake zilizowasilishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Hamza Hassan Juma, alisema umoja na mshikamano katika jamii unatoa fursa muhimu kwa viongozi wakuu wa nchi kutekeleza mipango, miradi ya maendeleo, kuwajengea mazingira bora, na kuwasaidia watu wenye ulemavu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**FUAD DAUD RENDY** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. **S0265/0022** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **CORNELIUS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/267707/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**HASSAN NASSOR MOYO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. **S1888/0053** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **PATRICK MISSION HIGH SCHOOL** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **:PHQ/DAR/KIN/267843/2024**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT Cap.117 R.E. 2019)**
**DEED POLL ON CHANGE OF NAME**

**BY THIS DEED, I** the undersigned **BENJAMIN KALIMANZILA MPILIPILI** a resident of Kyela, Tanzania. A natural born Tanzanian citizen **DO HEREBY ABSOLUTELY** denounce and abandon the use of my former names of **BENJAMIN MPILIPILI KALIMANZILA** as appearing in my National Identification (NIDA Card)and others **BENYAMIN M. KALIMANZILA** and **BENJAMIN K. MPILIPILI** as appearing in any of my other credentials used in any official transaction and in lieu therefore do assume as from the date hereof the name of **BENJAMIN KALIMANZILA MPILIPILI.**

AND in pursuance of such change of name as aforesaid I hereby declare that I shall at all times hereafter in all records, deeds and instruments in writing and in all actions and proceedings and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever use and sign the said name of **BENJAMIN KALIMANZILA MPILIPILI** as my name in lieu of the of the said names above captured renounced as aforesaid.

**AND I HEREBY AUTHORIZE** and request all persons to designate and address me by such assumed name of **BENJAMIN KALIMANZILA MPILIPILI** only.

**IN WITNESS WHEREOF** I have hereunder signed my assumed name of **BENJAMIN KALIMANZILA MPILIPILI** and have set my hand on this 25th day of November, 2024.

SIGNED and **DELIVERED** at Kyela before me by the said **BENJAMIN KALIMANZILA MPILIPILI,** who is introduced to me by **ELIZABETH KIWELU** in my presence on this 25th day of November, 2024.

SIGNED and DELIVERED at Kyela before me by the said BENJAMIN KALIMANZILA MPILIPILI who is ~~known to me personally or~~ introduced to me by Elizabeth Kiwelu in my presence on This 25th day of November, 2024.

DEPONENT



BEFORE ME:

Name: MIKE HONEST LYIMO Esq.

Address: P.O. Box 320, KYELA

Capacity: Commissioner for Oaths

Signature:

## TANGAZO LA KUPOTEA KADI YA GARI

Ndugu **DANIEL SILANGA MOLLEL** wa Mkoani ARUSHA amepotelewa na kadi ya gari yenye usajili namba **T412 AXL** aina ya **TOYOTA CORONA** Kwa yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi .Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/46435/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **WARDA HAMDANI SALIM** wa Kata ya Ipuli Mnadani Manispaa ya Tabora Mkoani Tabora amepotelewa na kadi ya gari yenye usajili namba **8592595** ya gari yenye usajili namba **T156 AHN** aina ya Scania,model 113,chassis namba **1130496** ambayo imepotea tangu mwaka 2022 na ametoa taarifa kituo cha kati Polisi mjini Tabora na kupatiwa jalada namba **TBR/PLR/N/017/2024.**Kwa yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi,Ofisi ya Serikali au awasiliane na muhusika kwa simu namba **0788980078.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**UPENDO AMOS MWANGUSA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA MITSUBISHI PAJERO YENYE USAJILI **T650 BHL** ILIYOPOTEA. KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/19134/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **OBWORI ALEX NYAMBANE** amepotelewa na kadi ya gari yenye usajili namba **T 616 CMS** aina ya – **SUBARU** yenye rangi **GREY** chassis number: **BP5076135,** -engine. number: **EJ200469744** Kwa yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi,Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/46231/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SADICK ANDREAS GONGO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE USAJILI **MC446 ALG.** KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI JALADA **PHQ/IRI/KIL/16993/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**RAMADHAN YUSUF MBWANA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE USAJILI **T146 CKV** ILIYOPOTEA KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/19035/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**MELAS ADRIAN MAKOBO,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC154CST,** Yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/55326/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AGAPTUS HERMAN JOSEPH** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA BLUE CARD YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 603 DYW,**AINA YA GARI NI **BMW SERIES** 3,CHASSIS NO.**WBAVA76060NL31037** KWA YOYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/MBE/MBE/40064/2024.**

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 29482 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GABRIEL ANTO RINGA**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY GRACE GABRIEL MUSHI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 19TH day of December, 2024.
Dated at KOROGWE this 28TH day of November, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 29837 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE PETER EZRA MSANGI**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**

1. **MARIAMU AMIRI DOLOO**
2. **JOSEPH PETER MSANGI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL Person Claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 3rd day of January, 2025.
Dated at KOROGWE this 28TH day of November, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 29835 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE AZARIA MOSES KISSE**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**

1. **ROSEMARY MICHAEL MAYOMBO**
2. **RICHARD MOSES KISSE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 03 day of January, 2025.
Dated at KOROGWE this 28 day of November, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 29345 OF 2024**

**IN THE MATTER OF ESTATE OF THE LATE SANKEY DAVID MWANJALI**

**AND**

**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY NELDA GEORGE KIMARO AND DEBORA DAVID MWANJALI**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 20 Day of 12..........................2024
Dated at Dodoma this 8th Day of NOVEMBER ................2024.

1ST PETITIONER    2ND PETITIONER

Presented for filling this ....04..... Day of ....12.......2024

RESIDENT MAGISTRATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha KAWE Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Na. MADAI 530 YA 2024**

**Jina la mdai: LK Microfinance (Kelvin Liberika)**

**Jina la Mdaiwa: i. MARY CHEREHANI ii. MWANAKHAMISI MDINI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa : i. Marry Cherehani ii. Mwanakhamisi Mdimi Wa Tatedo Goba**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba ( Eleza hapa habari za Madai) K**UJIBU DAI LA PESA KIASI CHA TSHS. 188,400/=**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 10 Mwezi 12 Mwaka 2024 Saa 8:30 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa Shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 28 Mwezi 11 Mwaka 2024.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
KAWE

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 29709/ 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE NAITI NELSON MWANKENJA**

**AND**

**In the matter of Application for Letters of Administration by**

**ALEX ALEX MWINUKA............................PETITIONER**

**GENERAL CITATION (RULE 75)**

All persons claiming to have interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to came and see the proceeding if they think fit before the grant of Probate (or letters of Administration) is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the18th day of December, 2024.
Dated at Kyela this 22rd day of December, 2024

SENNIOR RESIDENT MAGISTRATE
KYELA.

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 28199/ 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE THOMAS MARTIN THOMAS**

**AND**

**In the matter of Application for Letters of Administration by**

**ADELINA PHILIPO STEPHANO...............PETITIONER**

**GENERAL CITATION (RULE 75)**

All persons claiming to have interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to came and see the proceeding if they think fit before the grant of Probate (or letters of Administration) is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 16th day of December, 2024.
Dated at Kyela this 3rd day of December, 2024

SENNIOR RESIDENT MAGISTRATE
KYELA.

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 30482 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE FLORENCE KYUSA KUROSSO**

**AND**

**In the matter of Application for Letters of Administration by**

**CLAUDE HENRY KUROSSO..................PETITIONER**

**GENERAL CITATION (RULE 75)**

All persons claiming to have interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to came and see the proceeding if they think fit before the grant of Probate (or letters of Administration) is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 23rd day of December, 2024.
Dated at Kyela this 3rd day of December, 2024

SENNIOR RESIDENT MAGISTRATE
KYELA.

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Wabunge Korea Kusini kumwondoa rais Ikulu

**SEOUL,** Korea Kusini

HATIMAYE wabunge wa Korea Kusini, wapo katika mchakato wa kumwondoa madarakani Rais Yoon Suk Yeol, kwa kumpigia kura za kutokuwa na imani naye.

Usiku wa kuamkia juzi, Rais Yoon, alitangaza nchi hiyo kuwa katika sheria za kijeshi akidai kuna njama za kufanya mapinduzi kutoka kwa watu wanaoshirikiana na Korea Kaskazini.

Hata hivyo, wabunge walifanikiwa kuingia ndani ya jengo la bunge kwa kuruka ukuta baada ya eneo hilo kuzingirwa na wanajeshi ambao walizuia shughli zote za bunge.

Wabunge wa upinzani waliwasilisha hoja ya kutokuwa na imani na rais, na wanasubiri taratibu za kujadili kumalizika ili waanze kupiga kura.

Pindi muswada wa kumwondoa madarakani utakapopendekezwa, takriban theluthi mbili ya wabunge katika Bunge la Kitaifa lenye wajumbe 300 la Korea Kusini lazima wapige kura ili kupitisha hoja hiyo ya kutokuwa na imani na Yoon.

Katiba ya nchi hiyo inataka wabunge wasiopungua 200 kupiga kura na ifanyike ndani ya saa 72.

Hatua inayofuata ni kwa Spika wa Bunge Woo Won-sik kuitisha kikao ili hoja hiyo ijadiliwe.

Rais Yoon ametangaza Jumatano asubuhi kwamba ameondoa sheria ya kijeshi nchini humo saa chache baada ya kuitangaza.

Hatua hiyo inawadia baada ya wabunge 190 waliokuwapo bungeni kwa kauli moja kuzuia hatua hiyo.

Wakati akiondoa amri huyo, Rais Yoon alisema „Baada ya Bunge la Kitaifa kutaka kuondoa sheria za kijeshi, wanajeshi wa sheria za kijeshi wameondolewa. Nitakubali ombi la wabunge na kuondoa sheria ya kijeshi kupitia mkutano wa baraza la mawaziri.“

Baada ya kauli hiyo, chama kikuu cha upinzani nchini Korea Kusini kimemtaka Rais Yoon Suk Yeol kujiuzulu ama apigiwe kura ya kutokuwa na imani naye kutokana na hatua yake ya kutangaza sheria ya kijeshi katika taifa linaloamini demokrasia.

Mmoja wa wanachama waandamizi wa chama cha upinzani cha Democratic Party alisema ilibainika tangu awali kwamba Yoon hawezi kuendesha nchi hiyo kwa njia za kawaida.

Katika hotuba yake aliyoitoa juzi usiku, alielezea kuwepo kwa majaribio ya upinzani wa kisiasa kuhujumu serikali yake. BBC

# Nandi-Naitwah rais wa kwanza mwanamke kuiongoza Namibia

**WINDHOEK,** Namibia

MGOMBEA wa Chama cha SWAPO, Netumbo Nandi-Ndaitwah, amechaguliwa kuwa Rais wa Namibia baada ya kupata ushindi wa asilimia 57 wa kura zote.

Nandi-Naitwah, amekuwa rais wa kwanza mwanamke kuiongoza nchi hiyo baada ya kuchaguliwa kwa kura nyingi katika uchaguzi mkuu uliofanyika wiki iliyopita.

Tume ya Uchaguzi ya Namibia (ECN), ilitangaza matokeo hayo usiku wa kuamkia jana na kumtaja Nandi-Ndaitwah, kumshinda mpinzani wake kutoka Chama cha Patriots For Change (IPC), Panduleni Itula, ambaye amepata asilimia 25.5.

Hata hivyo, Itula na chama chake wameyakataa matokeo hayo wakisema hawatambui wakidai uchaguzi ulikumbwa na udanganyifu mwingi.

Nandi-Ndaitwah mwenye umri wa miaka 72, ataongoza kuitawala nchi hiyo ya kusini mwa Afrika yenye utajiri wa madini.

**Tume ya Uchaguzi ilieleza kuwa kati ya watu milioni 1.5 waliojiandikisha kupiga kura, karibu asilimia 77 walipiga kura kumchagua rais.**

Namibia imekuwa chini ya uongozi wa chama cha SWAPO tangu ilipopata uhuru wake mwaka 1990.

Zoezi la upigaji kura liliongezwa muda kutoka Novemba 27 hadi 30 baada ya kujitokeza matatizo ya kiufundi ikiwemo uhaba wa makaratasi ya kupigia kura.

Hatua hiyo ulichukuliwa baada ya watu kushindwa kupiga kura siku ya kwanza kutokana na kusubiri karatasi za kupigia kura kwa zaidi ya saa 12.

Chama cha IPC kilisema kwamba kitendo hicho kilifanywa kwa makusudi na kwamba hakitokubali matokeo.

Shirika moja la mawakili wa haki za binadamu kusini mwa Afrika lilikuwa mwangalizi wa uchaguzi, lilisema uhaba wa karatasi za kura uliojitokeza na kucheleweshwa kwa upigaji kulifanyika kimakusudi na lilitokea katika maeneo mengi.

Itula mwenye umri wa miaka 67 alisema wiki iliyopita kwamba uchaguzi huo ulikumbwa na mapungufu mengi. Aliongeza kwamba chama cha IPC kitapambana kwa kutumia njia zote za mchakato wa uchaguzi nchini humo kuhakikisha kwamba zoezi zima la uchaguzi limefutwa.

Msemaji wa chama cha IPC Imms Nashinge, akizungumza baada ya tangazo la matokeo lililotolewa na tume ya uchaguzi, alisema chama hicho kinashikilia msimamo wake wa kutokubali matokeo.

Tume ya Uchaguzi nchini Nambia ECN ilikiri kufeli katika maandalizi ya uchaguzi huo, ikiwamo upungufu wa karatasi za kura na baadhi ya kompyuta zilizotumika kuwasajili wapigakura kupata moto kupita kiasi na kushindwa kufanya kazi.

Tume ya Uchaguzi ilieleza kuwa kati ya watu milioni 1.5 waliojiandikisha kupiga kura, karibu asilimia 77 walipiga kura kumchagua rais.

"Raia wenzangu wa Namibia, uchaguzi huwa wenye ushindani kwa kawaida ila demokrasia inatutaka sote tuungane mara yanapotangazwa matokeo. Natoa wito kwa Wanambia wote wayakumbatie matokeo kwa umoja, maelewano na maridhiano," alisema mwenyekiti wa ECN Elsie Nghikembua baada ya kutangaza matokeo hayo. **DW**



Rais mteule wa Namibia, Netumbo Nandi-Ndaitwah, akikunja ngumi kama ishara ya ushindi baada ya kutangazwa kwa matokeo ya kura katika uchaguzi uliofanyika nchini humo. **PICHA: AP**

# Ugonjwa mpya waibuka DRC

**KINSHASA,** DRC

NAIBU Gavana wa Mkoa wa Kwango, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) Remy Saki na Waziri wa Afya wa nchi hiyo, Apollinaire Yumba, wameelezea kuzuka kwa ugonjwa usiojulikana Kusini Magharibi mwa nchi hiyo.

Walisema watu walioambukizwa na ugonjwa huo walikuwa na dalili za kuugua mafua makali, joto kali la mwili na kuumwa kichwa.

Kwa mujibu wa maofisa hao wa ngazi za juu wa DRC, timu ya madaktari imepelekwa katika kitengo maalum cha afya cha Panzi kuchukuwa sampuli na kuanzisha uchunguzi ili kutambua ugonjwa huo.

Kiongozi mmoja wa shirika la kiraia Cephorien Manzanza, aliliambia shirika la habari la Reuters kwamba hali hiyo inatiwa wasiwasi kufuatia kuongezeka kwa idadi ya walioambukizwa.

Mtaalamu mmoja wa magonjwa ya mlipuko kwenye eneo hilo, alisema wengi walioambukizwa ni kinamama na watoto.

HABARI MICHEZO

# GEITA GOLD YATOA ONYO CHAMPIONSHIP KWA 5G

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Geita Gold imetoa onyo kwa timu zote zinazoshiriki Ligi ya Championship kwa kuitwanga Greeen Warriors mabao 5-1 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumbu mkoani, Geita juzi na kuweka rekodi ya timu iliyopata ushindi mkubwa zaidi kwenye ligi hiyo.

Mabao ya Geita Gold katika mechi hiyo yalifungwa na Hamisi Ngoengo dakika ya 11 na 71, Andrew Sinchimba (dakika ya 29 na 68) na Pius Enosi akipigia msumari wa mwisho kwenye jeneza la Green Warriors dakika ya 90.

Ushindi huo unaifanya Geita Gold kujiimarisha katika nafasi ya pili, lakini ikiwa na pointi 26 sawa na kinara wa ligi hiyo, Mtibwa Sugar, zote zimecheza mechi 11, zimeshinda mechi nane, sare mbili na kupoteza mchezo mmoja kila mmoja.

**Kinachowatofautisha ni Mtibwa Sugar imefunga mabao 19 na kuruhusu mabao matano, kitu kinachoifanya kuwa juu ya Geita Gold ambayo imepachika mabao 18 na kuruhusu mabao sita wavuni kwake.**

Baada ya kipigo hicho, Green Warriors inabakia katika nafasi ya 12 ya kwenye msimamo wa Ligi ya Championship ikiwa na pointi 10 katika mechi 11 ilizocheza mpaka sasa.

Kwenye Uwanja wa Kambarage mkoani, Shinyanga, Stand United ilipata ushindi wa nyumbani wa mabao 2-1 dhidi ya Songea United kutoka Ruvuma.

Mabao ya Boniphace Shaaban na Emmanuel Manyanda yakliipa pointi tatu muhimu Stand United huku Nassor Katanga, akifunga bao la kufutia machozi kwa upande wa Songea United.

Ushindi huo unaipeleka Stand United iliyoshuka daraja kutoka Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21, kukamata nafasi ya tatu ya msimamo ikiwa na pointi 22, huku Songea United ikiwa kwenye nafasi ya saba na pointi zake 19.

Timu mbili zitakazomaliza katika nafasi ya juu zitapanda kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao huku itakayomaliza kwenye nafasi ya tatu na ya nne zitapambana kwenye michezo ya mtoano dhidi ya klabu kutoka Ligi Kuu.




Brasi bendi ya Jeshi la Wananchi la Tanzania (JWTZ), ikitumbuiza katika sherehe za Mahafali ya 19 ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere cha jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bunge kamili kuchuana Mombasa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MSAFARA wa Timu za Michezo za Bunge unatarajiwa kuondoka nchini kesho kuelekea jijini Mombasa, Kenya kwa ajili ya kushiriki mashindano ya 14 ya Mabunge ya Afrika Mashariki.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Mwenyekiti wa Klabu ya Bunge, Abbas Tarimba, alisema wataenda kushiriki mashindano mbalimbali yatafayofanyika kuanzia keshokutwa hadi Desemba 17, mwaka huu.

Tarimba alisema maandalizi ya kushiriki michuano hiyo yamefanyika vyema kwa wachezaji kukaa kambini kwa muda wa siku saba jijini hapa.

"Tumejiandaa vizuri kuelekea katika mashindano haya, tuliweka kambi hapa Dodoma na msafara unatarajiwa kuwa na watu 120, ikiwamo wabunge na wafanyakazi wa Bunge," alisema Tarimba.

Aliongeza alisema Bunge litashiriki katika michezo yote ambayo ipo kwenye mashindano hayo ikiwamo mpira wa miguu, mpira wa pete, kikapu, wavu, kuvuta kamba, gofu na vishale ambao ni mahsusi kwa wabunge wenye ulemavu.

"Wabunge pamoja na kutimiza kazi zao za kibunge wanahimizwa kufanya mazoezi ili kujenga miili na afya zao ili kufanya kazi za kibunge kwa ufanisi, michezo hii inatumika kuimarisha ushirikiano wa nchi za Afrika Mashariki, nchi zinazoshiriki ni Tanzania, Kenya, Rwanda, Burundi, Uganda, Sudan Kusini, Somalia na DR Congo," Tarimba alisema.

Naye, Meneja wa Klabu ya Bunge, Seif Gulamali, alisema vifaa vya michezo vimepokelewa kwa ajili ya kushiriki mashindano hayo huku akiwaomba Watanzania waliopo Kenya wajitokeze kuwaunga mkono wabunge wao.

## Mabao 195 yaingia kambani Ligi Bara

**Na Adam Fungamwango**

JUMLA ya mabao 195 yamefungwa katika michezo 98 ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo imechezwa mpaka sasa.

Idadi hiyo ni ndogo ukilingalishwa Ligi Kuu msimu ulipita ambapo hadi kufikia raundi ya 13, jumla ya mabao 223 ilikuwa imefungwa.

Kwa mujibu wa dawati la takwimu za michezo Nipashe, kati ya mabao 195 yaliyofungwa ya jumla ya wachezaji 116, magoli 25 ni ya mikwaju ya penalti, huku 170 yakifungwa kwa njia ya kawaida.

Hata hivyo, kati ya mabao hayo, manne ni ya kujifunga, ambapo wachezaji walipachika mipira kwenye lango lao katika harakati za kutaka kuokoa.

Wachezaji hao ni Fred Tangalo wa KMC, akijifunga katika mchezo kati ya timu yake dhidi ya Azam FC, ikipoteza kwa mabao 4-0, Kevin Kijili wa Simba akifanya hivyo katika mchezo wao dhidi ya Simba, ikipoteza kwa bao 1-0, Yannick Bangala wa Azam akijifunga katika mchezaji ambao timu yake ilishinda mabao 3-1 dhidi ya Dodoma Jiji wiki hii na Dickson Mhilu wa Dodoma Jiji, akijifunga katika mchezo huo huo, timu yake ikichapwa mabao 3-1 dhidi ya Wanalambalamba.

Jumla ya penalti 31 zimetolea mpaka sasa kwenye ligi, 25 zikiwekwa wavuni na sita zikiota mbawa, nne zikipanguliwa na makipa, na mbili zikikoswa na wachezaji wenyewe.

## Rombo Marathon Festival kumekucha

**Na Grace Mwakalinga**

WANARIADHA na wadau wa michezo kutoka maeneo mbalimbali nchini wanatarajiwa kushiriki mbio za Rombo Marathon Festival zitakazofanyika Desemba 23, mwaka huu, kwenye Uwanja vya Kilombero, wilayani Rombo, Kilimanjaro.

Mwenyekiti wa Bodi ya Rombo Marathon Festival, Prof. Adolph Mkenda, Mbunge wa Jimbo la Rombo, ambaye pia ni Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, alisema ni msimu wa tatu, mbio hizo zinafanyika.

Mkenda alisema mbio hizo zitawahusisha wanariadha maarufu na wananchi wanaopenda michezo kama sehemu yao ya kujenga afya na kufurahi pamoja.

"Ni duru ya tatu sasa tunafanya hii Rombo Marathon Festival, ambazo zitakuwa na shughuli mbalimbali kama vyakula vya kienyeji, ndafu choma, kwa hiyo licha ya kuwa washiri- ki watafanya riadha, lakini pia watakula na kunywa, nawahamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika mbio hizi ambazo zitafika hadi kilomita 10, kutakuwa na fursa watu kujionea uzuri wa misitu yetu ya asili ,"alisema Mkenda.

Aliongeza marathon hiyo imekuwa na mchango mkubwa katika kuinua vipaji vya wananchi wa Rombo na kutoa fursa kufanyika michezo mingine kama mashindano ya mpira wa miguu kupitia Mkenda Cup.

## ZISIKUPITE

**FERGUSON ATAKIWA FOREST**
KLABU ya Nottingham Forest inajiandaa kuwasilisha dau la kumnunua mshambuliaji wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Evans Ferguson mwenye umri wa miaka 20 Januari. (***Football Insider***)

**ANORLD AKARIBIA MADRID**
REAL Madrid inataka kumsajili beki wa Liverpool na England, Trent Alexander-Arnold mwenye umri wa miaka 26 kwa uhamisho wa bure. ***(Telegraph)***

**ZUBIMENDI NA LIVERPOOL**
LIVERPOOL inapanga kufanya uhamisho wa pauni milioni 91 Januari kwa beki wa Bournemouth mwenye umri wa miaka 21, Milos Kerkez na kiungo wa Real Sociedad na Hispania, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 25. (***Teamtalk***)

**NICO WILLIAMS ANYATIWA**
ARSENAL, Chelsea, Liverpool na Tottenham Hotspur ni miongoni mwa klabu zinazomwania winga wa Athletic Bilbao mwenye umri wa miaka 22, Nico Williams. (***Athletic)***

**BARCELONA YAMNYATIA ISAK**
KLABU ya Barcelona inamfuatilia mshambuliaji wa Newcastle United na Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 25. (***Caught Offside)***

**MAN UNITED YAMTAKA RAUM**
MANCHESTER United ina nia ya kumsajili beki wa RB Leipzig na Ujerumani, David Raum mwenye umri wa miaka 26, na mshambuliaji wa Juventus na Uturuki, Kenan Yildiz mwenye miaka 19. (***Sky Germany***)

**...YAWASILIANA PIA NA DAVIES**
KLABU ya Manchester United imewasiliana na beki wa Canada, Alphonso Davies mwenye umri wa miaka 24, ili kutathmini nia yake ya kujiunga na klabu hiyo wakati mkataba wake na Bayern Munich utakapokamilika msimu ujao. (***Team Talk)***

**LEICESTER YATAKA MSHAMBULIAJI**
KLABU ya Leicester City ina nia ya kuimarisha safu yake ya ushambuliaji na ina mpango wa kumsajili mshambuliaji mpya dirisha la uhamisho wa wachezaji litakapofunguliwa Januari. (***Football Insider***)

**DALOT AGOMBEWA LA LIGA**
BARCELONA itashindana na Real Madrid kumnunua beki wa Manchester United na Ureno, Diogo Dalot, iwapo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 ataonesha nia ya kuondoka Old Trafford. (***Caught Offside***)

**TEN HAG ATAJWA LEIPZIG**
KOCHA wa zamani wa Manchester United, Erik ten Hag ananyatiwa na klabu ya RB Leipzig. (***Sun, via Sky Germany)***

**DIALLO KUONDOKA UNITED**
WINGA wa Ivory Coast, Amad Diallo mwenye umri wa miaka 22, huenda akaondoka Manchester United Januari. ***(Express)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SLOT ASHANGAZWA MUSTAKABALI WA MOHAMED SALAH LIVERPOOL

**●●●** Kocha huyo amecheka kuhusu taarifa za nyota huyo huku mwenyewe ikisemekana...

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Arne Slot amecheka kuhusu taarifa za mustakabali wa Mohamed Salah katika klabu hiyo.

Salah aliifungia Liverpool bao la pili dhidi ya Manchester City Jumapili lakini baadaye akawaambia mashabiki kwamba anahisi kama mchezo huo unaweza kuwa wa mwisho dhidi ya Man City kwenye uwanja wa Anfield anapokaribia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake.

Alipoulizwa kuhusu maoni yake, Slot alichagua kuizungumzia City na kwamba kikosi cha Pep Guardiola kinaweza kushushwa daraja kwa sababu ya mashtaka 115 dhidi yao.

**"Labda Mo anajua zaidi kuhusu mashtaka 115 kwa hivyo anatarajia haitakuwa kwenye Ligi Kuu msimu ujao," aklisema Slot huku akicheka.**

"Jibu la kuchosha huwa ni lile lile, hapa sio mahali pa mimi kuongelea kuhusu mkataba wa Mo, labda nimeshasema mengi kwa utani nilioufanya."

Ripoti za hivi karibuni zilidai Salah anasumbuliwa na hali ya sintofahamu inayoendelea kuhusu mustakabali wake, akibainisha nia yake ya kusaini mkataba wa mwaka mmoja wa nyongeza.

Slot aliulizwa kama kuna hatari kwamba Liverpool wanaweza kumtegemea sana Salah ambaye tayari ana mabao 13 na asisti 11 katika mechi 20 pekee kwenye michuano yote.

"Kidogo, lakini kwa sababu tu ni binadamu na ilimtokea msimu uliopita anaweza kupata jeraha pia," alisema Slot.

"Federico Chiesa amekuwa na mwanzo mgumu kwenye klabu kwa sababu ya majeraha kwa hiyo hatufanyi hivyo kuwa na mbadala wa Mo.

"Kitu kizuri ni kwamba Harvey Elliott anazidi kuwa fiti zaidi na amecheza nafasi hii mara nyingi pia."



# AMORIM: KUNA DHORUBA INAKUJA MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

RUBEN Amorim amewaonya mashabiki wa Manchester United kwamba „dhoruba itakuja" akimaanisha nyakati ngumu licha ya mwanzo wake mzuri kama kocha mkuu.

Amorim hajapoteza katika michezo yake mitatu ya uongozi na aliiongoza United kupata ushindi wao mkubwa zaidi wa ligi tangu 2021 kwa ushindi wa 4-0 dhidi ya Everton Jumapili.

"Ningependa kusema mambo tofauti, lakini sina budi kusema tena, dhoruba itakuja," alisema Amorim

"Sijui kama utatumia msemo huo, lakini tutakuwa na wakati mgumu na tutapatikana kwenye baadhi ya michezo, hilo nalijua kwa kuwa nawafahamu wachezaji wangu na najua soka na nafuatilia soka.

"Kwa hiyo tuzingatie kila mchezo, juu ya uchezaji, kile tunachopaswa kuboresha, kujaribu kushinda michezo. Na hilo ndilo lengo. Najua ni vigumu sana kuwa kocha wa Manchester United na kusema mambo haya katika mikutano na waandishi wa habari.

"Tunataka kushinda wakati wote, hata iweje, tutajaribu kushinda, lakini tunajua kuwa tuko katika hatua tofauti, ukilinganisha na Arsenal."

Wakati wachezaji wa Amorim bado wanajifunza kuhusu mfumo wake wa kimbinu, Amorim pia anajifunza kuhusu United.

Kocha huyo Mreno amekuwa kwenye kibarua hicho kwa muda wa wiki tatu tangu achukue nafasi ya Erik ten Hag, na amekiri umakini na kazi inayokuja na kuinoa moja ya klabu kubwa duniani imemshangaza.

# Barcelona haitasajili Januari

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA inatarajiwa kuelekeza nguvu katika dirisha la usajili la Januari katika kuongeza mikataba, badala ya kutumia soko kutafuta wachezaji wapya.

Kuna sehemu katika kikosi zinaweza kuimarishwa, lakini Sport inabainisha kuwa hakuna mpango wa kufanya usajili mwezi ujao.

Na ingawa Flicks anafahamu ni wapi uwanjani unahitaji kuboreshwa, hajadai sura zozote mpya kwa sasa, huku majira ya kiangazi yakiwa yametengwa kwa ajili ya harakati hiyo ya kuajiri.

Lengo namba moja la Barcelona ni kufanikisha usajili wa Dani Olmo na Pau Victor.



Upungufu wa kifedha wa klabu hiyo ulimaanisha njia pekee ya kufikia hilo Agosti, ambayo ilikuja baada ya kuanza kwa msimu, ilikuwa ni kufutwa kwa usajili kwa Andreas Christensen wakati wa jeraha lake.

Zaidi ya hayo, Barcelona wanataka kutangaza kuongezwa kwa mkataba waliokubaliwa kwa Pedri na Gavi hadi angalau 2029.

Barcelona hawataki kumuacha mchezaji yeyote wakati wa Januari, huku Ansu Fati ndiye pekee anayeweza kuondoka akiwa amekumbwa na majeraha tangu aliporejea kutoka kwa mkopo ambao haukufanikiwa msimu uliopita katika klabu ya Brighton & Hove Albion.



# Madrid wajipanga kwa Alexander-Arnold

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imeripotiwa kujiweka sawa katika harakati za kutaka kumsajili beki wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold.

Alexander-Arnold anatajwa kuwa miongoni mwa mabeki bora zaidi wa pembeni duniani lakini hatma yake ndani ya Liverpool imekuwa na sintofahamu kubwa kutokana na mkataba wake kuelekea mwisho.

Hiyo ina maana kwamba anaweza kupatikana kwa uhamisho wa bure mwishoni mwa msimu ikiwa hakuna makubaliano mapya ya kusalia Anfield yatafikiwa.

Alexander-Arnold ataruhusiwa kufanya mazungumzo rasmi na kusaini makubaliano ya awali ya mkataba na klabu yoyote itakapofika Januari.

Vinginevyo, Liverpool pia watakuwa na chaguo la kujaribu kutafuta fedha wakati wa dirisha la uhamisho, nafasi yao ya mwisho kuleta ada ya uhamisho ikiwa beki wa kulia ataondoka.

Kwa mujibu wa gazeti la Telegraph wababe hao wa Hispania wana nia ya kumsajili Alexander-Arnold kwa uhamisho wa bure, na hivyo kuondoa mbinu ya ada ya aina yoyote katika wiki chache zijazo.

Madrid walichukua mtazamo sawa na kutaka kumnunua beki wa kati Leny Yoro wakati wa majira ya joto.

Alphonso Davies anayelengwa kwa muda mrefu anaweza kupatikana kama mchezaji huru msimu huu wa majira ya joto kutokana na mkataba wake unaomalizika Bayern Munich, huku klabu hiyo pia haikulipa ada ya uhamisho wa Kylian Mbappe.

Alexander-Arnold tayari ni rafiki wa karibu na nyota wa Madrid, Jude Bellingham na kukiri kwa mchezaji huyo kuwa anataka kuweka historia ya kuwa beki wa kwanza wa pembeni kushinda tuzo ya Ballon d'Or kulichukuliwa na gwiji wa Liverpool, Jamie Carragher ikiwa ni dalili ya kuondoka klabuni hapo.

## Fadlu aficha silaha, Manula abakia Dar

INATOKA UKURASA 24

tia watakuwa ugenini.

"Tunatakiwa tuwe vizuri zaidi katika eneo la kuzuia huku tukijiepusha kufanya makosa mengi. Tumefanya mazoezi ya kuimarisha safu ya ulinzi na nafasi ya kiungo wa kukaba kwa sababu tunacheza ugenini, pia tunatakiwa kushambulia kwa haraka tukiwa na mpira na kurudi mapema," Fadlu, kocha huyo raia wa Afrika Kusini alisema.

Alisema kwa ushirikiano wa pamoja kati ya mabeki, viungo na washambuliaji, kama wakifanya majukumu ya kulinda na kushambulia kwa pamoja, anaamini wataibuka na ushindi katika mchezo huo muhimu.

"Najua mechi itakuwa ngumu kwa sababu Algeria ni moja kati ya nchi zenye ligi bora Afrika, huku bingwa wake mara nyingi huwa hatabiriki, timu yoyote ile inaweza kuwa bingwa tofauti na nchi nyingine ambazo baadhi ya timu zimejitwalia ufalme," aliongeza Fadlu.

Nahodha wa Simba, Mohamed Hussein ‚Zimbwe Jr', alisema wamekwenda kupambana na ajili ya timu yao pamoja na nchi kwa ujumla.

"Tunakwenda kupambana kwa ajili ya Simba na Tanzania, ni mechi muhimu na ngumu sana, kila timu ilipata ushindi katika mchezo wa kwanza. Wachezaji tunafahamu ugumu wa mchezo, ila hatuwaogopi kwa sababu wako kwao kwa sababu Simba ni wazoefu kucheza na timu za Afrika Kaskazini. Hatuna wasiwasi hata kama watakuwa kwao mbele ya mashabiki wao, kupata ushindi ugenini inawezekana, tumeshawahi kushinda nje ya uwanja wetu wa nyumbani," alisema beki huyo wa kushoto wa Simba na Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Wakati huo huo, Manula ameshindwa kuendelea na safari baada ya kupata matatizo ya kiafya dakika chache kabla ya kuanza safari ya kuelekea Algeria.

Maneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema Manula ameshindwa kuendelea na safari hiyo kutokana na sababu hizo, hivyo kikosi kiliondoka na wachezaji 21 badala ya 22 ambapo sasa makipa waliosafiri ni Moussa Camara na Ally Salim.

# FEI TOTO HAKAMATIKI ASISTI, MABAO YA PENALTI LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum ‚Fei Toto', anaongoza kwa kufunga na kutoa pasi nyingi za mwisho katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea.

Pia nyota huyo wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), anaongoza kwa kufunga mabao mengi kwa penalti.

Hadi kufikia raundi ya 13 ya Ligi Kuu Tanzania Bara, mchezaji huyo ametoa asisti tano na kuwa juu ya orodha ya wachezaji walitoa pasi za mwisho nyingi ambazo zilizaa mabao.

Fei Toto pia anaongoza kwa kufunga mabao mengi ya penalti, akiwa amefanya hivyo mara tatu.

Kiungo huyo wa zamani wa Yanga ambaye amefunga mabao manne katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, matatu ameyafunga kwa penalti katika mchezo kati ya timu yake dhidi ya KenGold, uliochezwa, mechi iliyochezwa Oktoba 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam wenyeji wakishinda mabao 4-1, lingine ikiwa ni Novemba 23, mwaka huu, alipofunga bao pekee kwenye Uwanja huo wa Azam ikishinda 1-0 dhidi ya Kagera Sugar.

Kwa mujibu wa dawati la takwimu za michezo la Nipashe, wanaofuatia kwa kufunga mabao mengi ya penalti, Jean Ahoua na Leonel Ateba, ambao wote wamefunga mabao mawili ya penalti kila mmoja na Ogochukwu Morice wa Tabora United ambaye naye amepachika penalti mbili.

Ahoua alifunga katika mchezo kati ya timu yake dhidi ya Dodoma Jiji, ikishinda bao 1-0, na dhidi ya KMC, timu yake ikishinda mabao 4-0, Ateba akipachika penalti zake, katika mchezo dhidi ya Coastal Union zikitoka sare mabao 2-2 na dhidi ya Pamba Jiji, likiwa bao pekee kwenye mechi hiyo, huku Ogochukwu akifunga dhidi ya Pamba Jiji timu yake ikishinda bao 1-0 pamoja na Mashujaa, ikishinda pia bao 1-0.

Wakati Fei Toto, akiwa na ‚asisti' tano, wachezaji Ahoua wa Simba na Salum Kihimbwa wa Fountaina Gate, wana ‚asisti' nne kila mmoja.

Jumla ya wachezaji saba wanashika nafasi ya tatu kwa kutoa asisti nyingi, kila mmoja akitoa tatu.

Wachezaji hao ni Stephane Aziz Ki wa Yanga, Josephat Bada na Ande Koffi wa Singida Black Stars, Yacouba Songne na Heritier Makambo wa Tabora United, Salehe Masudi wa Pamba na Ismail Mgunda wa Mashujaa.




Kiungo wa Pamba Jiji FC, Salehe Masoud (kulia), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa KenGold ya Mbeya katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza juzi. Pamba Jiji ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# Coastal yawaza 'Top Four'

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 2-1 katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi Tanzania Prisons mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha wachezaji wa Coastal Union wamepania kumaliza ligi katika nafasi nne za juu, imeelezwa.

Bao la dakika za nyongeza lililofungwa na Maulid Shaaban liliihakikishia Coastal Union pointi tatu muhimu ambazo zimewapaisha mpaka nafasi ya tisa katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kufikisha pointi 16.

Akizungumza na Nipashe jana, Shaaban, alisema ushindi huo ni muhimu sana kuwapo katika kukoleza nia yao ya kutaka kumalizi ligi kwenye nafasi nne za juu.

„Nimefurahi sana kuiwezesha timu yangu kupata ushindi, kama wachezaji tunatamani sana kumaliza katika nafasi za juu na ndio lengo letu kuwa kwenye ‚Top 4'," alisema Shaaban.

Nyota huyo amesema kila siku zinavyozidi kwenda ligi imekuwa ngumu lakini wataendelea kupambana kuhakikisha wanafanya vizuri katika kila mechi.

„Kama wachezaji tunahitaji kujituma sana, Ligi imekuwa ngumu na tunaelekea kumaliza mzunguko wa kwanza, tutapambana katika kila mchezo kwa sababu tunatamani sana kumaliza kwenye nafasi nne za juu msimu huu," alisema Shaaban.

# Michezo



Nipashe Alhamisi Desemba 5, 2024

**Amorim: Kuna dhoruba inakuja Man United** UKURASA 22



Wachezaji wa Simba, Fabrice Ngoma (kushoto) na Moussa Camara, wakiwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam usiku wa kuamkia jana, tayari kwa safari ya kuelekea Algeria katika mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya wenyeji CS Constantine ya nchini humo. **PICHA: SIMBA SC**

## Fadlu aficha silaha, Manula abakia Dar

**Na Adam Fungamwango**

HUKU Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, akisema hatafanya mazoezi yoyote ya mbinu wakiwa Algeria ili kutowapa nafasi wapinzani wao, CS Constantine kufahamu mfumo watakoutumia, kipa, Aishi Manula, ameugua ghafla na kulazimika kubakia Tanzania.

Manula alikuwa ni sehemu ya wachezaji waliotakiwa kuelekea Algeria kwa ajili ya kuwavaa wenyeji CS Constantine katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa Jumapili nchini humo.

Fadlu aliliambia gazeti hili badala yake atakuwa na kazi ya kusimamia mazoezi ya kuwaweka fiti kimwili wachezaji wake kwa kuchezea mpira tu.

Kocha huyo alisema maandalizi yote muhimu ya mchezo huo yalimalizikia wakiwa Tanzania, kinachofanyika ugenini ni kuondoa uchovu wa safari.

"Tutakachokifanya ni kuhakikisha wanakuwa sawa upande wa utimamu wa mwili tu, kwa sababu ni hatari kufanya mazoezi ya mbinu ya mchezo huo kwa sasa. Tulimaliza mazoezi ya kimbinu pamoja na kuyafanyia kazi mapungufu na ubora wa wapinzani wetu tukiwa Tanzania.

Huku yatakuwa ni mazoezi ya kawaida tu ya kuweka miili sawa kwa sababu macho yatakuwa mengi kututazama, siwezi kufanya mazoezi ya kimbinu au chochote kile kinatachowafanya wapinzani wetu hata kuhisi tunacheza vipi," alisema kocha huyo.

Aliongeza moja kati ya maandalizi waliyoyafanya pamoja na kufanyia kazi wapinzani wao ni kuimarisha safu ya ulinzi pamoja na kiungo wa ulinzi kwa kuzinga-

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga: Hatuna wasiwasi

## ●●● Kikosi chawasili salama na kutamba wamefuata furaha...

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI kikosi cha Yanga kikitua salama nchini Algeria, uongozi wa timu hiyo umesema wako kamili na hawana wasiwasi wowote kuelekea mechi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wenyeji MC Alger utakaochezwa keshokutwa mjini Algiers.

**Yanga itashuka katika mechi hiyo ya pili ya hatua ya makundi ikiwa na kumbukumbu ya kufungwa mabao 2-0 na Al Hilal ya Sudan, mechi ili yochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam wiki iliyopita.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Msemaji wa Yanga, Ali Kamwe, alisema kikosi chao kimesafiri vyema na kila mchezaji yuko katika hali nzuri kwa ajili ya kuipambania timu yao.

Kamwe alisema wanatarajia kukamilisha programu ya mazoezi kuelekea mechi hiyo itakayokuwa chini ya benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Sead Ramovic.

"Sisi uzuri tunakwenda Algeria mjini, tukifika pale benchi letu la ufundi litaangalia tunaanzia wapi, tunasiku chache zimebaki kabla ya mechi yetu, „ alisema Kamwe.

Aliongeza wanafurahi kuona mechi yao itachezwa kwenye Uwanja wa Julai 5, 1962 baada ya maombi ya kuhamishiwa kwenye Uwanja wa Ali la Pointe kukataliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Inaelezwa MC Algers iliamini kuupeleka mchezo huo ulioko katika Mji wa Douera uliopo kilomita 19 kutoka jijini Algers wangekuwa kwenye mazingira bora zaidi ya kupata ushindi.

Taarifa kutoka CAF zinasema mchezo huo utachezwa kwenye uwanja uliopangwa na kupitishwa na CAF awali.

CAF imewafungia MC Algers kucheza michezo minne bila mashabiki kutokana na makosa ya utovu wa nidhamu yaliyoonyeshwa na mashabiki wao katika mechi ya mwisho ya kufuzu hatua hiyo ya makundi waliyocheza dhidi ya US Monastir ya Tunisia.

Wakati huo huo kiongozi aliyetangulia Algeria aliliambia gazeti hili maandalizi ya kupokea msafara wa timu yao yamekamilika na wanatarajia kila kitu kitakwenda vizuri.

Chanzo hicho kilisema kwa sasa Yanga haina hofu ya kucheza ugenini kutokana na uzoefu waliokuwa nao katika kukabiliana na changamoto za aina yoyote.

"Tunatarajia kuipokea timu mchana huu (jana mchana) na mchezo utachezwa kama ilivyopangwa awali kwenye uwanja wa Julai 5, tumejiandaa kuwapa furaha mashabiki wetu," alisema kiongozi huyo.

Chanzo hicho kiliongeza Yanga inatarajia kushuka uwanjani kuwakabili Waarabu hao kwa utulivu na tahadhari, kwa sababu wanajua kila timu inahitaji pointi tatu za kujiimarisha kwenye kundi lao.

Aliongeza wachezaji wote walioko katika mpango kuelekea mechi hiyo wamesafiri na wanaamini watapambana kusaka matokeo chanya.

Kabla ya kuanza safari hapa nchini, Ramovic aliweka wazi amekiandaa kikosi chake kucheza kwa tahadhari kwa sababu malengo yao ni kufanya vizuri katika mechi hiyo ya Kundi A.

Yanga wamepania kupata ushindi katika mchezo huo ili kufufua matumaini ya kucheza hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara wanaburuza mkia katika msimamo wa kundi lao linaloongozwa na Al Hilal inayofundishwa na Mkongomani Florent Ibenge.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >